# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2020 HADI 2025) KWA KIPINDI CHA JULAI HADI DISEMBA, 2024

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Mahali ilipo

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ya Pangani ni miongoni mwa Wilaya nane **(8)** na Halmashauri kumi na moja **(11)** zinazounda Mkoa wa Tanga. Kijiografia Wilaya ya Pangani iko kusini mwa Jiji la Tanga, kwa upande wa Mashariki inapakana na Bahari ya Hindi, Magharibi Wilaya ya Handeni, Kaskazini Wilaya ya Muheza na Kusini Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

Aidha, Wilaya ipo **Km 47** kutoka Makao Makuu ya Mkoa, ambapo Wilaya inaukubwa wa eneo la Kilometa za Mraba (**Km$^2$**) **1,830.8**, na Sehemu kubwa iko ukanda wa Pwani na Mji wake Mkuu ni Pangani ambapo mto Pangani unaingia Bahari kuu ya Hindi.

### 1.2 Hali ya hewa

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ipo kwenye ukanda wa Pwani, katika mwinuko kati ya **Mita 0 – 100** kutoka usawa wa bahari. Aidha, Wilaya hupata mvua za Vuli, Masika na mchoo zenye wastani wa kati ya **mm 1000 – mm 1500** kwa mwaka.

**Vuli -** (Oktoba - Disemba)

**Masika** - (Machi - Mei)

**Mchoo** - (Julai - Agosti)

### 1.3 Utawala na Idadi ya watu

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ya Pangani inaundwa na Tarafa **4,** Kata **14,** Vijiji **33** na Vitongoji **96**. Kwa mujibu wa Sensa ya watu na Makazi ya Mwaka **2022**, Wilaya ina jumla ya watu **75,642** kati ya hao wanaume **38,203** na wanawake **37,439** na kaya zipo **20,254** zenye ukubwa wa wastani watu **3.7** kwa kaya.

**Jedwali na.1 Muundo wa Wilaya Kiutawala**

| NA. | TARAFA | IDADI YA KATA | IDADI YA VIJIJI | IDADI YA VITONGOJI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Madanga | 4 | 9 | 32 |
| 2. | Pangani Mjini | 3 | 3 | 10 |
| 3. | Mwera | 5 | 15 | 39 |
| 4. | Mkwaja | 2 | 6 | 15 |
| **Jumla Kuu** | | **14** | **33** | **96** |

### 1.4 Viongozi wa kuchaguliwa na Masuala ya Utumishi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ya Pangani inao Viongozi mbalimbali ambao wamepatikana kwa njia ya uchaguzi ambao ni Pamoja na Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Madiwani wa Kata. Aidha, eneo la Uajijibikaji na utendaji limeendelea kuimarishwa kuhakikisha huduma bora kwa wananchi inapatikana.

#### 1.4.1 Viongozi wa kuchaguliwa ndani ya Wilaya

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ina Tarafa **4**, Kata **14**, Vijiji **33** Vitongoji **96** na Jimbo **01** la Uchaguzi. Halmashauri ya Wilaya ya Pangani inaundwa na Madiwani **19** Madiwani **14** wa Kata, Madiwani **05** wa Viti Maalum, na Mbunge **01** wa Jimbo) ambao wote wanatokana na Chama Cha Mapinduzi.

#### 1.4.2 Masuala ya uwajibikaji na utendaji kazi

**Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 110 (a)** inasisitiza juu ya kuhakikisha kuwa Madaraka kwa Umma yanabaki kuwa ndio msingi wa Utawala katika nchi, Aidha, **Ibara ya 112 (a) ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi,** inaelekeza kusimamia nidhamu, uadilifu, uwazi, uzalendo wa kitaifa, moyo wa kujitolea na uwajibikaji miongoni mwa Viongozi na Watumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kipindi cha Julai – Disemba, 2024. Halmashauri imepokea Watumishi wa ajira mpya **85**. Ikiwa ni Madereva **02,** Watendaji wa Kijiji **08,** Waendesha Ofisi **05,** Watendaji wa Kata **02**. Idara ya Biashara Viwanda na Uwekezaji ajira mpya **04.** Kitengo cha Utamaduni, Sanaa **na** Michezo **01,** Idara ya Maendeleo ya jamii ajira mpya **01,** Kitengo cha Maliasili na Utalii ajira mpya **03,** Idara ya Afya ajira mpya **58** na Idara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ajira mpya **01.** Hata hivyo, Halmashauri imeendelea kusimamia nidhamu kwa Watumishi na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma. Pia idara inaendelea na maandalizi ya Bajeti ya mshahara (PE) kwa Mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri, imeendelea kusimamia utekelezaji wa Vikao mbalimbali vya kisheria vya ngazi ya Halmashauri, Kata **14** na Vikao na Mikutano Mikuu ya Vijiji **33** ili kuimarisha Demokrasia katika ngazi za Wananchi waliopo ngazi za chini.

Pia, Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri chini ya Idara ya Ujenzi na Mipango imeendelea kusimamia ujenzi wa jengo la Utawala makao Makuu ya Halmashauri mradi upo katiika hatua ya ujenzi wa ukuta, nguzo mlalo, na sakafu ya juu upande wa pili wa jengo. Ununuzi wa Samani za Ofisi Pamoja na ujenzi wa nyumba 02 za Wakuu wa idara Makao Makuu ambayo ipo katika hatua ya manunuzi upande wa vifaa na fundi.

M**heshimiwa Mwenyekiti**, kwa kipindi cha bajeti 2024/2025 Julai hadi Disemba, 2024. imeendelea kusimamia utekelezaji wa maslahi ya watumishi ambapo Maandalizi ya kuwapandisha Vyeo na kuwabadilishia Vyeo/ Kada Watumishi linaendelea ili kuwapa motisha Watumishi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya inaendelea kuhakikisha kuwa huduma bora kwa Wananchi inapatikana katika maeneo sahihi ili kuleta heshima kwa Serikali.

**1.5 Hali ya Kiuchumi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Shughuli za Kiuchumi katika Wilaya ya Pangani ni biashara ndogondogo, Uvuvi, Kilimo na Ufugaji. Uchumi wa Wananchi wa Pangani kwa sehemu kubwa unakua kutokana na uwepo wa fursa ya bahari ambayo uwezeshaji wa shughuli za Uvuvi. Mpango mzuri wa Serikali ya awamu ya sita katika kutumia fursa za uchumi wa Buluu unakwenda kupanua Sekta ya Uvuvi kwa Wananchi wa Pangani kupitia fursa ya upatikanaji wa boti za kisasa ambazo zitawezesha kufanyika kwa Uvuvi wenye tija kubwa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya imeweza kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Serikali ndani ya Wilaya ya Pangani. Sekta za Afya, Elimu, Maji, Barabara, Utawala, Nishati, kuwezesha makundi ya uzalishaji Maji na shughuli zingine za maendeleo kwa Wananchi katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2024/2025.

**2.0 Hali ya Ulizi na Usalama**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wilaya inaendelea kuimarisha Usalama wa Raia wake na Mali zao ili kudumisha Umoja, Mshikamano, Amani na Utulivu ambazo ni tunu za Taifa letu.

**2.1 Usalama wa Raia na Mali zao**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hali ya Ulinzi na Usalama katika Wilaya ya Pangani ni shwari, hakuna tishio kubwa la usalama lililotokea katika kipindi hiki. Wananchi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na Usalama wanaendelea kubaini wahalifu na matukio ya kihalifu na kuchukua hatua. Aidha, changamoto iliyopo ni ya makosa ya ukatili yanayotokea katika jamii na kufikishwa katika vyomo vya usalama hasa ubakaji na ulawiti. Katika kukabiliana na changamoto hii hatua zinazochukuliwa na vyombo vya usalama ni kuendelea kuwabaini wahusika wa matukio hayo ili sheria iweze kuchukua hatua.

**2.2 Hali ya upatikanaji wa Chakula**

**Mheshiwa Mwenyekiti**, Idadi ya watu Wilaya ya Pangani ni watu **75,642** hivyo Mahitaji ya Chakula kwa mwaka yanakadiriwa kuwa tani **15,753** ambapo tunatarajia kuvuna tani **59,111.6** za chakula hivyo hali ya chakula ni ya utoshelevu.

**2.3 Hali ya Kisiasa** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Kisiasa Wilaya ya Pangani inaridhisha kwani vyama vya siasa vimekuwa na mahusiano mazuri na Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ya Pangani imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii na Kiuchumi kupitia Sekta zilizopo ndani Wilaya. Sekta hizo ni kwa upande wa Halmashauri ni pamoja na; Sekta ya Fedha, Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo, Utawala, Maendeleo ya Jamii, Maliasili na Biashara na kwa upande wa Taasisi cni ya Serikali Kuu ni

Maji (Tanga UWASA, RUWASA), TARURA, TRA, TFS TANESCO na Bandari. Utekelezaji wa Sekta hizo ni kama ifuatavyo: -

# UTEKELEZAJI WA ILANI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI DISEMBA, 2024 KUPITIA SEKTA MBALIMBALI ZA HALMASHAURI

## 3.0 SEKTA YA FEDHA

Halmashauri inaendelea kuongeza ubunifu katika upatikanaji wa rasilimali fedha inayohitajika ili kuwezesha utoaji huduma kwa wananchi wa Pangani.

### 3.1 Mapato ya Halmashauri kwa Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 imekisia kukusanya mapato kiasi cha **Shilingi 2,311,229,000.00**. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2024 Halmashauri imekusanya **Shilingi 962,128,733.00** sawa na asilimia **42%** ya lengo kwa mwaka. Aidha, kati ya mapato haya Mapato lindwa ni **Shilingi 395,108,609.00** na Mapato yasiyolindwa ni **Shilingi 567,820,124.**

## 4.0 SEKTA YA ELIMU

### 4.1 ELIMU MSINGI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Idara ya Elimu Msingi imetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025) kwa Ufanisi mkubwa. Kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2024 Idara imefanikiwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa asilimia 90%

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Idara imefanikiwa kuweka misingi imara ya usimamizi wa Fedha za Elimu bila malipo na Fedha za Miradi ya Ujenzi ya uboreshaji wa kada ya ualimu (GPE/TSP) na PLASCO ambapo fedha hizo kwaajili ya ujenzi wa Vyumba vya madarasa na Ujenzi wa Matundu ya vyoo kwa shule za Msingi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ibara ya 80 (1a) ya Ilani ya CCM inaelekeza kujenga na kukarabati Miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule. Idara ya elimu msingi imepokea fedha kiasi cha **Shilingi 210,700,000.00,** ikiwa ni fedha za uboreshaji kada ya ualimu (GPE /TSP) pamoja na PLASCO kiasi cha **Shilingi 30,000,000.00** kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 ambazo zimepokelewa nje ya bajeti na utekelezaji unaendelea, mradi upo hatua za awali za upatikanaji wa Wazabuni wa vifaa na Mafundi umekamilika, mradi unasubiri Cheti cha msamaha wa Kodi kutoka TRA ili kazi ianze.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Aidha, kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi waliomaliza darasa la saba, imeongezeka kutoka **86.4%** (2022) hadi **87%** mwaka 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ii. Ibara 80(2b) - Kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa., Mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wa Awali yamefanyika kwa Walimu **36**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mafunzo endelevu kwa Walimu Awali (KKK) yamefanyika jumla ya Walimu **32** walipatiwa mafunzo, lengo ni kuongeza umahiri kwa Walimu ili kuhakikisha wanafunzi wote wa Awali wanajua KKK kabla ya kujiunga na darasa la kwanza.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** iii. Ibara 80(2a) - Kuendeleza mpango wa kutoa Elimu bila malipo kwa Shule za msingi ili kuwezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea bila kikwazo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Jumla ya **Shilingi 111,044,567.00** zimepokelewa kwa ajili ya kugharamia Elimu bila malipo ambapo fedha hizi zimewezesha kugharamia shughuli za kielimu ikiwemo michezo mitihani, ukarabati mdogo na ununuzi wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ibara 80(2c) - Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kiasi cha **Shilingi 3,700,000.00** zimetumika kugharamia utoaji wa chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Fedha hizo zimesaidia kuboresha lishe za Wanafunzi katika kitengo Maalum Shule ya msingi Funguni pamoja na Shule jumuishi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

i. Ibara 80(2f) Idara imetekeleza kwa vitendo kupitia uimarishaji wa masomo ya maadili, uzalendo wa kitaifa na uraia kwa shule zote Wilayani Pangani.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri imeanzisha klabu za ushauri nasaha kwa shule zote za msingi ili kuimarisha maadili Shuleni.Pia vikundi vya skauti vimeanzishwa na kusimamiwa katika shule **10** ambazo ni Funguni, Pangani, Kimang'a, Bushiri, Kikokwe, Mwera, Mivumoni, Masaika na Mwembeni.

## 4.2 SEKTA YA ELIMU SEKONDARI

**Mweshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ina shule **14** za sekondari zenye usajili wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kati ya shule hizo kumi (**10**) zinamilikiwa na serikali ambazo ni Bushiri, Funguni, Mwera, Kilimangwido, Kipumbwi, Mkwaja, Tongani, Jumaa Aweso, Masaika na Pangani halisi. Shule nyingine (**4**) zinamilikiwa na taasisi binafsi ambazo ni Istiqaama Pangani, Al- Hijra, Capuchin Boys na Franciscan Girls .

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha mwezi Julai–Disemba,2024 kazi zifuatazo zilitekelezwa na Idara;

- ✓ Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya walimu (2 in 1) katika sekondari ya Masaika kwa ufadhili wa Sequip yenye gharama ya **Shilingi 98,000,000.00**
- ✓ Kuendelea na ujenzi wa shule mpya ya kata kwa ufadhili wa Mradi wa kuboresha Elimu ya Sekondari **(SEQUIP**) awamu ya tatu katika kata ya Pangani Mashariki yenye thamani ya **Shilingi 584,280,029.00**
- ✓ Kuendelea na umaliziaji wa mabweni **02** katika sekondari ya Funguni yenye gharama ya **Shilingi 62,545,238.20** fedha kutoka serikali kuu.

- ✓ Kuhudhuria kikao cha tathmini ya lishe Wilaya kilichoazimia shule zote kutoa chakula kwa wanafunzi na kupunguza matumizi ya fimbo kwa wanafunzi kwa kutumia njia mbadala katika kuadhibu**.**
- ✓ Kufanya ufatiliaji wa kila wiki wa **KPI (Key Performance Indicator**) katika shule zote za sekondari na kuwaslisha taarifa kwa Katibu Tawala Mkoa Alhamisi ya kila wiki.
- ✓ Kufuatilia ukusanyaji wa fedha ya Hostel na Hali ya lishe (chakula), afya na mazingira katika shule zote za sekondari
- ✓ Kufanya kikao kazi cha mwezi cha Idara juu ya mikakati na majukumu mbalimbali ya utekelezaji kwa ngazi ya Ofisi ya Afisa Elimu na Ngazi ya Shule.
- ✓ Kuhudhuria kikao cha maandalizi ya mtihani wa upimaji wa Kidato cha Pili 2024 na mtihani wa kumaliza Kidato cha Nne 2024 Tanga.
- ✓ Kuandaa na kufanya mtihani wa Pre-National Mkoa kwa Kidato cha Pili na Kidato cha Nne.
- ✓ Kuendesha mtihani wa upimaji wa Kidato cha Pili 2024 ulioanza tarehe 28/10/2024 na kumalizika tarehe 06/11/2024.
- ✓ Kuendesha mtihani wa kumaliza Kidato cha Nne 2024 ulioanza tarehe 11/11/2024 na kumalizika 27/11/2024
- ✓ Kushughulikia taarifa mbalimbali za Idara ya Elimu Sekondari, madeni ya walimu na wazabuni.
- ✓ Kutoa ushirikiano kwa wakaguzi kutoka ofisi ya mkaguzi mkuu wa serikali na TAMISEMI waliokuja kufanya ukaguzi na kufatilia ujenzi wa shule mpya Pangani Mashariki na nyumba ya walimu shule ya sekondari Masaika.
- ✓ Mapokezi ya fedha kiasi cha **Shilingi 160,000,000.00** shule ya Sekondari Pangani Halisi kwa ajili ya umaliziaji wa mabweni **02** na Bwalo **01**.
- ✓ Kufanya uchaguzi wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza 2025. Jumla ya wanafunzi **1310 (wav 605 was 705)** walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule za Sekondari **10**.
- ✓ Kufanya Mtihani wa kumaliza muhula wa Pili 2024 kwa Kidato cha Kwanza na tatu.
- ✓ Kutoa matokeo na ripoti kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na tatu na zoezi la kufunga shule tarehe 6/12/2024.

**Jedwali na.1 Ujenzi wa Miundombinu katika shule za Sekondari**

| NA | AINA YA MIUNDOMBINU | FEDHA ZILIZOPOKELEWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA | HATUA YA UJENZI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa shule mpya ya kata ya Pangani Mashariki. | 584,280,029.00 | 357,078,000.00 | Majengo yote yapo hatua ya umaliziaji. |
| 2 | UJenzi wa nyumba moja ya walimu (2 in 1) shule ya sekondari Masaika | 98,000,000.00 | 41,050,000.00 | Ujenzi upo hatua ya kuezeka na umaliziaji. |
| 3 | Umaliziaji wa Bweni Funguni Sekondari | 62,545,238.20 | 45,560,000.00 | Uwekaji wa milango ya alluminium chooni upande wa wasichana na wavulana |
| 4 | Umaliziaji wa mabweni 2 na Bwalo 1 shule ya sekondari Pangani Halisi. | 160,000,000.00 | 0 | Hatua ya kununua vifaa. |
| | **JUMLA** | **1,146,625,267.2** | **443,688,000.00** | |

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 Halmashauri ilipokea na kutumia kiasi cha **Shilingi 272,365,533.00** na kutumika kiasi cha **Shilingi 272,365,533.00** kwa Miezi sita ikiwa ni fedha za elimu bila malipo kwaajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za shule za Sekondari.

## 5.0 SEKTA YA AFYA

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sekta ya Afya kupitia vitengo vyake imetekeleza shughuli mbalimbali za Afya tiba na kinga kama inavyoelezewa katika taarifa ifuatayo hapo chini;

**Ibara 83(b)** - Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi kulingana na mahitaji katika ngazi zote za utoaji wa huduma za Afya nchini;

**Utekelezaji**, Upatikanaji wa dawa ni kwa wastani wa 95.04% na vifaa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi ni kwa asilimia 91% Huduma zimetolewa katika Hospitali ya Wilaya **01**, Vituo vya Afya **03**, Zahanati **17** za Halmashauri ujenzi wa Zahanati mpya mbili uko hatua za mwisho kukamilika.

ii. **Ibara 83(3)** - Kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ikiwemo mifuko ya bima za afya (NHIF na CHF) ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote.

**Utekelezaji**, Mfuko wa CHF katika halmashauri ya Wilaya ya Pangani ni 7% ya wanufaika wa mfuko wa CHF, NHIF inaendelea kutumika na Uhamasishaji kwa wananchi kujiunga na mfuko wa NHIF wananchi unaendelea.

iii. **Ibara 83(g)** Kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika hospitali **28** za rufaa ngazi ya Mkoa, Hospitali za Halmashauri za Wilaya **125** kwa kukamilisha ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya kutolea huduma (Majengo, Vifaa na Watumishi).

**Utekelezaji**. Kiasi cha **Shilingi 900,000,000.00** Milioni zimetumika kukarabati hospitali kongwe ya Halmashauri ya Wilaya Pangani

Aidha, Upanuzi wa huduma katika hospitali ya Wilaya ya Pangani umefanyika, kwa kujenga jengo la Wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU), na kiasi kilichotumika **Shilingi 250,000,000.00** Ujenzi wa ICU umekamilika na ukarabati wa Hospitali ya Wilaya umekamilika.

**Ibara 83(m) -** Kuhamasisha jamii umuhimu wa matumizi ya vyandarua vilivyowekwa dawa na upuliziaji wa viatilifu ukoko katika kuta za nyumba.

**Utekelezaji,** Vyandarua vimegawiwa kwa wajawazito **659** walio fika kliniki kwa mara kwanza na Watoto **614** wanaokuja kwenye chanjo ya SURUA (MRI), Uhamasishaji na uelimishaji jamii umuhimu wa matumizi sahihi ya Vyandarua vilivyowekwa dawa ni endelevu.

vi. **Ibara83(u)** - Kuimarisha huduma za Afya ya Mama na Mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya na kuzifanya rafiki kwa Wanawake, Wanaume na Vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya Afya ya Uzazi na Mtoto, huduma tembezi na Mkoba.

**Utekelezaji**, Huduma za Afya ya Mama na Mtoto zinatolewa katika vituo vyote **22** ikiwemo hospitali ya Wilaya **01**, vituo vya Afya vitatu **03** na Zahanati **17** za Serikali na Zahanati **01** ya Asasi ya kidini.

**Mheshimiwa mwenyekiti**, Aidha huduma ya dharura kwa Wajawazito na Watoto Wachanga imekuwa ikitolewa kupitia mpango wa M-mama katika kata zote **14** za Wilaya ya Pangani, kuna baadhi ya Kata wana madereva taxi ngazi ja jamii ambao hutumika kusafirisha Watoto na Wajawazito wenye dharura, Sehemu zingine ambao hawana dereva taxi ngazi ya jamii huwa wanatumia gari ya kusafirisha Wagonjwa (ambulance).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Huduma tembezi na Mkoba zimekuwa zikitolewa katika vituo vyote **22** vilivyopo Wilayani. Aidha huduma rafiki kwa vijana inayohusu elimu ya Afya ya Uzazi imekuwa inatolewa katika vituo **04** vya kutolea huduma, mikakati inaendelea kufanyika ili vituo vyote viwe vinatoa huduma rafiki kwa Vijana kwa kushirikiana na Serikali Pamoja na Wadau (USAID Afya Yangu na AMREF HEALTH AFRICA).

iii. **Ibara 83(x)-** Kuboresha Miundombinu ya kutolea huduma za macho, Afya ya kinywa na Meno, Koo, Masikio, Pua na Vifaa tiba na Watumishi wenye ujuzi katika ngazi zote za kutolea huduma za Afya

**Utekelezaji,** Serikali imenunua (complete dental Chair) 3 ambazo Hospitali ya Wilaya Pangani wamepewa moja, Vituo vya Afya vya Mkalamo na Mwera nao wamepata kiti **01**, Pia wametoa Dental X ray ya kisasa pamoja na kufanya ukarabati wa chumba chakutolea huduma za Kinywa na Meno kuifanya Ofisi hiyo kuwa ya kisasa zaidi na kutoa huduma bora kwa Wananchi wengi zaidi. Watumishi **02** walipata mafunzo kuhusu upimaji wa Maambukizi ya VVU kipima cha marudio kwa Mama Wajawazito na Wanaonyonyesha.

viii. **Ibara 83 (y)**- Kuimarisha ushirikiano na Sekta binafsi katika utoaji wa huduma za Afya.

**Utekelezaji.** Katika Halmashauri ya Pangani katika Sekta ya Afya kuna wadau mbalimbali tunaoshirikiana nao katika utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika maeneo mbalimbali.

Baadhi ya wadau hao ni pamoja na shirika la AMREF Africa, Tanzania Health Support Program (THPS), SIKIKA, na vituo binafsi vinavyotoa huduma ya afya kwa wananchi.

x.**Ibara 86(b)**- Kufanya tathmini ya kila mwaka kuhusu hali ya Lishe na tathmini maalum kila baada ya miaka mitano na hatimaye kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na Wananchi wenye Afya bora na uwezo wa kuchangia ipasavyo katika Shughuli za Maendeleo ya Taifa lao;

**Utekelezaji**, Halmashauri imeendelea kufanya vikao vya kila robo vinavyojadili hali ya Utekelezaji wa viashiria vya lishe vilivyo ainishwa katika ilani ya chama tawala ambavyo mpaka sasa vikao vikao viwili (2) vya tathimini ya Utekelezaji wa afua za lishe katika mwaka fedha 2023/2024 tayari vimefanyika.

Aidha, hali ya udumavu katika halmshauri ya Wilaya ni asilimia 0%.

xi.**Ibara 86(d)**- Kupunguza kwa asilimia 50 viwango vya upungufu wa damu kwa Wanawake walio katika umri wa kuzaa yaani miaka (**15 – 49**); na kuongeza kiwango cha unyonyeshaji wa maziwa ya Mama pekee kwa Watoto chini ya miezi sita ili ifikie zaidi ya asilimia 50%.

**Utekelezaji**, Katika kipindi cha Miezi mitatu (Oktoba-Disemba, 2024) Hali ya upungufu wa uwingi wa damu kwa wanawake waliokatika umri wa kuzaa ni asilimia 0.7%.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hali ya unyonyeshaji wa maziwa ya Mama pekee kwa watoto wachanga walio na umri chini ya miezi sita ni asimia **98.53**%.

**Mweshimiwa Mwenyekiti**, Aidha, Elimu ya afya na lishe imeendelea kutolewa kwa Wanawake walio katika umri wa kuzaa, wanaonyesha kwa kutumia njia mbalimbali kama vile kutumia vyombo vya habari, Mikutano ya Vijiji na kwa kutumia Wataalam waliopo vituo vya kutolea huduma za afya.

xii.**Ibara 86(h)**- Kuongeza na kuwajengea uwezo wataalam wa afya kwa ajili ya kutoa huduma za lishe katika ngazi za Mikoa, Halmashauri pamoja na Vituo vya kutolea huduma za Afya.

**Utekelezaji**, Tumefanikiwa kutoa mafunzo kwa wataalam **30** (12Me,18Ke) kutoka katika Vituo **22** vya kutolea huduma za Afya ya utambuzi na matibabu ya utapiamlo mkali kwa Watoto chini ya miaka mitano.

Aidha, wamefundishwa namna ya kutengeneza chakula dawa kwa kutumia vyakula vinavyopatikana katika mazingira wanayoishi.

**ix.Ibara 83(z) -** Kuimarisha mfumo wa upelekaji wa fedha moja kwa moja kwenye akaunti za vituo vya kutolea huduma za Afya ngazi ya msingi kwa kushirikisha Wadau wote wanaotekeleza Afua za Afya.
**Utekelezaji,** Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ina jumla ya Zahanati **17**, Vituo vya Afya **03** na Hospitali ya Wilaya **01** zenye usajili kamili na akaunti namba na pia zinapelekewa fedha moja kwa moja kwenye akaunti zao.

**Ibara 88(h)**- Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi na unyanyapaa.

**Utekelezaji**, Programu za uelimishaji kwa kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya **23**, Huduma Mkoba, mikutano pamoja na radio Pangani, zinaelimisha kuhusu afya na upimaji wa hiari pia elimu inatolewa ili kuondoa unyanyapaa kwa jamii kwa kushirikiana na shirika la UZIKWASA, THPS na Idara ya Afya, Ustawi wa jamii na lishe.

xiv. **Ibara 88(i)**- ufuatiliaji wagonjwa walioacha kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU unafanyika katika vijiji.

**Utekelezaji**. Ufuatiliaji wagonjwa walioacha kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU unafanyika katika Vijiji **33** kwa kuwafikia kwa njia ya simu na pia kuwatembelea majumbani na kuwapa huduma

za tiba na matunzo kwa ufadhili wa shirika la THPS, na waliopatikana walielimishwa zaidi na kuwekwa katika programu maalumu ya ufuatiliaji na umezaji wa Dawa za kufubaza makali ya VVU.

iv. **Ibara 83(l)** - Kuajiri wataalam wa kutosha wenye ujuzi na kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi wa sekta ya afya.

**Utekelezaji:** Kupitia kibali cha ajira Cha mwaka 2023, Halmashauri ya wa Wilaya Pangani tumepata watumishi wapya **58** wa kada mbalimbali za Afya.

## 6.0 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Idara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya Ibara 23 ambayo inaielekeza Halmashauri kupambana na Umasikini na Kuwezesha Wananchi Kiuchumi;

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Utekelelezaji wa majukumu kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 ni kama ifuatavyo; -

i. Kuhamasisha uundaji na usajili wa vikundi vya kijamii vya kiuchumi ambapo jumla ya vikundi **120** vimeundwa na kusajiliwa kwa mchanganuo ufuatao; vikundi vya wanawake **54**, vikundi vya vijana **48**, vikundi vya walemavu **48**.

**ii.** Kusajili Vikundi vya huduma ndogo za kifedha **22** vyenye jumla ya wanachama **660**

iii. Halmashauri imetenga na kutoa mikopo kwa vikundi **29**. Ambapo Wanawake vikundi **11** Vijana vikundi **10**, Walemavu vikundi **08** Mkopo wa thamani ya **Shilingi 254,901,081.00**

### 6.1 TASAF

**6.1.1 Kupambana na Umaskini na Uwezeshaji wa Wananchi KiuchumiIbara ya 26(n):** Kuboresha kasi ya utekelezaji Awamu ya Tatu ya TASAF ili kuwafikia wananchi masikni katika vijiji/mitaa yote kwa kutekeleza miradi ya kutoa ajira za muda, kukuza Uchumi wa Kaya na kuendeleza rasilimali watu.

### 6.2 Hali ya Utekelezaji,

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika Wilaya ya Pangani TASAF awamu ya tatu inatekelezwa katika Vijiji vyote **33**.

**Utekelezaji wa shughuli za TASAF ulifanyika kama ifuatavyo;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Idadi ya Kaya zilizopatiwa ruzuku ya kuongeza kipato cha Kaya kwa lengo la kukuza uchumi hadi kufikia Disemba, 2024 ni jumla ya wanufaika **7,760** ambapo Wanawake **4,389** na Wanaume **3,371**. Aidha, **3,240** ni idadi ya walengwa wanao kadiriwa kunufaika na ruzuku hiyo. Pia, huduma ya Utoaji wa ruzuku umefanyika na kuhawilishaji. Wananchi mawenufaika kwa kupatiwa ruzuku ya msingi jumla ya **Shilingi 858,749,748.00** imetolewa kama rukuzu kwa Kaya zilizopo katika mpango kwa njia ya taslimu na mtandao na

kiasi cha **Shilingi 57,211,440.00** kimetolewa kama fedha za uwezeshaji na usimamizi kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Vijijini.

## 7.0 SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

### 7.1 Sekta ya Kilimo

**Mweshimiwa Mwenyekiti**, Wilaya ya Pangani ina misimu miwili ya mvua ambayo ni msimu wa Vuli na msimu wa Masika.
**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wilaya ya Pangani ina misimu mikuu miwili ya mvua ambayo ni msimu wa Vuli na msimu wa Masika.

#### 7.1.1 Hali ya Mazao ya chakula

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kipindi cha Mwezi Julai- Disemba, 2024 Wilaya ililenga kulima hekta **13,916** za mazao ya chakula na matarajio ni kuvuna tani **76,964** hadi kufikia Disemba, 2024 hekta **8,193.4** zililimwa sawa na asilimia **87** kama inayoonekana kwenye jedwali:

**Jedwali na. 1, Uzalishaji wa Mazao ya Chakula**

| **MALENGO** | | | **UTEKELEZAJI** | |
|---|---|---|---|---|
| **Zao** | **Eneo(ha)** | **Mtarajio ya Mavuno (Tani)** | **Eneo (Ha)** | **Mavuno tarajiwa (Tani)** |
| Mahindi | 7331 | 13929 | 2,932.4 | 4300.7 |
| Mpunga | 386 | 311 | 0 | 0 |
| Kunde | 380 | 266 | 190 | 77.0 |
| Muhogo | 5490 | 59841 | 4,941 | 40242.2 |
| Ndizi | 189 | 1669 | 130 | 611.1 |
| Viazi vitamu | 140 | 948 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **13,916** | **76,964** | **8,193.4** | **45231.0** |

### 7.1.2 Hali ya chakula

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Idadi ya watu Wilaya ya Pangani ni watu **75,642** hivyo Mahitaji ya chakula kwa mwaka yanakadiriwa kuwa tani **16,753** ambapo tunatarajia kuvuna tani **59,111.6** za chakula hivyo hali ya chakula ni ya utoshelevu.

**7.1.3 Uzalishaji wa mazao ya biashara, Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kipindi Julai-Disemba, 2024 tumelenga kulima jumla ya hekta **23,505** za mazao ya biashara na matarajio ya lengo ni kuvuna tani **27,799**. Ambapo kwa kipindi hiki, zimelimwa jumla ya hekta **22,532** ambapo tumevuna tani **3,654.68** za mazao kama inavyoonekana kwenye jedwali.

**Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya biashara**

| **MALENGO** | | | **UTEKELEZAJI** | |
|---|---|---|---|---|
| **Zao** | **Eneo (ha)** | **Makadirio ya Mavuno (Tani)** | **Eneo (Ha)** | **Mavuno (Tani)** |
| Nazi | 6770 | 16896 | 6770 | 1043.53 |
| Mkonge | 9425 | 8156 | 9425 | 2,393.57 |
| Alizeti | 192 | 132 | 50 | 50 |
| Ufuta | 1023 | 849 | 200 | 165.98 |
| Korosho | 6075 | 1751 | 6075 | 0 |
| Pamba | 20 | 15 | 12 | 1.6 |
| **Jumla** | **23505** | **27799** | **22532** | **3,654.68** |

### 7.2 Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kitengo cha Mifugo na Uvuvi inajukumu la kusimamia uzalishaji wa mazao ya Mifugo na mazao ya Uvuvi, kusimamia Miundo mbinu ya Mifugo na kusimamia Sheria na Kanuni zinazoongoza Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kitengo cha Mifugo na Uvuvi inajukumu la kusimamia uzalishaji wa mazao ya Mifugo na mazao ya Uvuvi, kusimamia Miundombinu ya Mifugo na kusimamia Sheria na Kanuni zinazoongoza Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

**Muhtasari wa utekelezaji wa Malengo ya Kitengo kipindi cha Julai – Disemba, 2024**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha mwezi Julai– Disemba, **2024** kitengo kimetekeleza majukumu yafuatayo;

i. Kusimamia ubora na kuongeza uzalishaji wa Mazao ya Mifugo ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 jumla lita **352,062** za maziwa zilikusanywa katika vituo vya

kukusanyia maziwa (MCC) vya Pangani, Mwera na Mivumoni na kuuzwa kwenye kiwanda cha Tanga Fresh
kwa ajili ya usindikaji na kuongezwa thamani. Aidha, jumla ng'ombe na mbuzi **639** walichinjwa na kuzalisha Kilo **37,864** za nyama na vipande **639** vya ngozi ambapo thamani ya mazao yote kwa ujumla ni Tsh. **623,703,600.00** kama inavyoonekana kwenye jedwali

| **MAZAO** | **UZALISHAJI** | **THAMANI (Tsh)** |
|---|---|---|
| Maziwa (Lita) | 352,062.00 | 281,649,600.00 |
| Nyama (Kilo) | 37,864.00 | 340,776,000.00 |
| Ngozi (Vipande) | 639.00 | 1,278,000.00 |
| **Jumla** | | **623,703,600.00** |

ii. Kusimamia manunuzi ya ng'ombe wa mkopo kutoka TADB**.** Benki ya TADB imefanikiwa kuwakopesha wafugaji wadogo **33** wa ng'ombe wa maziwa kwa masharti nafuu ambapo jumla ya ng'ombe **51** wamekopeshwa kwa thamani ya **Shilingi 130,000,000.00** (Milioni mia moja na thelathini) kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa Maziwa. Aidha, Shirika la **Land or Lakes** kupitia mradi wake wa **TI3P** limetoa ruzuku ya **25%** ya mkopo huu sawa na **Shilingi 32,500,000.00** ambapo kila ng'ombe aliekopwa atalipiwa jumla ya **Shilingi 637,254.90**

iii. Kutoa elimu kwa njia ya redio kwa wafugaji juu ya ufugaji bora na wenye tija, kuzingatia Sheria mbalimbali za Mifugo, umuhimu wa chanjo mbalimbali za Mifugo na utunzaji wa Mifugo.

iv. Elimu ya ufugaji bora wa mifugo imetolewa kwa wafugaji **2356**, elimu hiyo imetolewa kupitia wataalamu wa mifugo waliopo kwenye Kata na Vijiji na mikutano mbalimbali.

v. Jumla ya ng'ombe **3,875** wamepata chanjo ya homa ya Mapafu (CBPP), chanjo ya Kichaa cha Mbwa **412** na chanjo ya mdondo kwa kuku **8,337,** chanjo ya ndui kwa kuku **6,725** na kuku **2,665** wamepata chanjo ya mafua (Infectious Coryza).

vi. Ng'ombe **45,675** mbuzi **75,412** na kondoo **5,126** wameogeshwa kwa dip na kunyunyiziwa ng'ombe **18,239**, mbuzi **6,889**, kondoo **7,101** kwa kutumia majosho yaliyopo Mivumoni, Msaraza, Mtango na Mikinguni.

vii. Jumla ya ng'ombe **440** wenye thamani ya **Shilingi 286,000,000.00** na Mbuzi/Kondoo **145** wenye thamani **Shilingi 10,440,000.00** waliuzwa kupitia Minada ya Mkalamo na Stahabu.

### 7.3 Sekta ya Uvuvi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kipindi cha mwezi Julai– Disemba, 2024 kitengo kimetekeleza majukumu yafuatayo;

i. Kupitia Mashamba Darasa ya ukuzaji viumbe maji yaliyopo Msaraza (**02**), Vijana **23** kupitia mpango wa serikali wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) wamepatiwa mafunzo ya vitendo juu ya unenepeshaji kaa.
ii. Taasisi ya Mwambao kwa kushirikiana na wanajamii wa kijiji cha Kikokwe Kata ya Bweni walifanikisha utengenezaji wa matumbawe bandia (Reef balls) **100** ambayo ambayo tayari yamekwisha wekwa bahari ili kuongeza mazalia ya samaki na kulinda mazingira.
iii. Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi ya Mwambao na CFMA ya PAMBWEBO zimeendelea kufanya doria za kustukiza za mara kwa mara baharini na kuendelea kudhibiti uvuvi haramu.

iv. shirika la IUCN kwa ufadhili wa ubalozi wa Ireland nchini Tanzania wanatekeleza mradi wa Bahari Mali Project, ambapo katika kipindi cha miezi sita (6), Vikundi viwili **02** vya Upendo group

### 7.4 Sekta ya Ushirika

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmasahuri ya Wilaya ya Pangani ina jumla ya Vyama vya Ushirika **19** vikiwemo Vyama vya Kuweka na kukopa (SACCOS) **07**, Vyama vya Kilimo na Masoko (AMCOS) **06** na Vyama vingine (Other Co-operatives) **06**. Jumla ya wanachama katika Vyama vya Ushirika ni **2,227** ikiwemo Ke **649** na Me **1,264.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, tuna Jumla ya Hisa (Shares) **Shilingi 146,670,000.00** katika Vyama vya Ushirika na Akiba za wanachama (Savings) ya Jumla ya Kiasi **Shilingi 1,334,182,783.00** na Amana (Deposits) **Shilingi 2,686,578.00** na mikopo iliyotolewa (Loan Issued Commulatives) hadi kufikia kipindi cha Disemba, 2024 ni Jumla ya **Shilingi 167,226,600.00** na kua na baki ya Mikopo (Loan outstanding balance) **Shilingi 929,234,471.15**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa upande wa Vyama vya Kilimo na Masoko (AMCOS) hadi kufikia Julai, 2024, Vyama hivi vimefanikiwa kuuza korosho ghafi kupitia Soko la awali **Kg 28,825** ambako Wakulima walifaidika pamoja na Halmashauri kuingiza kipato.

## 8.0 SEKTA YA BIASHARA, VIWANDA NA UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji ni Idara Mpya iliyoundwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 ikiwa ni Idara yenye vitengo viwili.

- Kitengo cha Biashara na Masoko.
- Kitengo cha Viwanda na Uwekezaji.

## 8.1 MALENGO YA IDARA YA BIASHARA VIWANDA NA UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Malengo makuu ya Idara hii ni kusimamia kanuni na taratibu za utoaji wa leseni za biashara, pia kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ili kuwawezesha kufanya biashara yenye mafanikio. Pia, kitengo kinahamasisha uanzishwaji wa viwanda na uendelezaji wa viwanda vilivyopo, Kuhamasisha uwekezaji na kusimamia wawekezaji waliopo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wakati wa utekelezaji majukumu, Idara imefanikiwa katika mambo yafuatayo;

i. Kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo 7 vya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali.
ii. Kufanikiwa usajili wa makampuni **08** ya watu binafsi (private Companies).
iii. Kusajili majina 0 ya biashara na utoaji wa leseni za Biashara 4 za kundi 'A' kwa kushirikiana na BRELA.
iv. Kutoa leseni za Biashara, leseni **394** za Biashara zenye thamani ya **Shilingi 32,183,000**
v. Leseni **48** za vileo yenye thamani ya **Shilingi 1,814,000** zimetolewa.

## 9.0 MALIASILI NA HIFADHI YA MAZINGIRA
## 9.1 UTANGULIZI
**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni suala muhimu kwa kuwa mazingira ni mtambuka na uhusiano wake na maendeleo ya Sekta nyingine ni mkubwa. Athari za kutokutunza

na kuhifadhi mazingira husababisha Sekta nyingine kushindwa kuzalisha kikamilifu na hivyo kuongeza umaskini.

Katika Ibara ya 234, Ilani inaeleza shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kupitia Ilani ya uchaguzi kwa kipindi cha miaka 5 (2015- 2020). Aidha, Ibara ya 235 inaelekeza shughuli ambazo zitatekelezwa kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa miaka mitano ijayo (2020- 2025).

## 9.2 Usimamizi wa maliasili na hifadhi ya mazingira

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** shughuli zifuatazo zimetekelezwa;

i. Kutoa elimu kwa wananchi juu ya utekelezaji wa sheria za usimamizi wa Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira katika Sekta za Misitu, Ufugaji Nyuki na Wanyamapori pamoja na hifadhi ya Mazingira.
ii. Kufanya doria shirikishi kwa kushirikiana kwa pamoja na watumishi wa Serikali Kuu (TFS) pamoja na Wananchi kwa kufuata taratibu na sheria. Aidha, Doria hizi zilifanyika kwenye misitu yote ya Hifadhi za Taifa na vijiji na ile Matajiwazi.

### 9.2.1 UVUNAJI WA MISITU

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika maeneo ambayo siyo ya hifadhi zilifanyika huduma kwa wateja waliojisajili kufanya biashara ya mazao ya misitu (Mbao, Mkaa, Kuni, Nguzo, Nyasi, Ukindu n.k) na maeneo ya binafsi; huduma hizo ni pamoja na kusimamia leseni zilizotolewa baada ya kikao cha mwaka cha uvunaji kilichoketi tarehe 25/06/2024 chini ya Uenyekiti wa Mhe. Mkuu wa Wilaya ambapo maeneo ya vijiji yanayovunwa ni Mseko, Mtonga, Mtango, Kwakibuyu, Kigurusimba na Mkwaja. Bado Kitengo kinahimiza matumizi ya Nishati Safi na Salama.

### 9.2.2 UPANDAJI MITI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wilaya ya Pangani ilijiwekea lengo la kupanda miche ya Miti **1,500,000** kila mwaka. kuanzia Julai hadi Disemba, 2024 jumla ya miche ya Miti iliyopandwa ni wastani wa miche **729,150** katika maeneo mbalimbali kama vile Vyuo, Magereza, BMU kwenye Mikoko, Wananchi, Shule za Msingi na Sekondari Pamoja na Wadau wa Maendeleo. katika maeneo mbalimbali yakiwemo yale ya hifadhi ya Mikoko na kando ya ukuta wa Mto Pangani ambao unaendelea kujengwa ikiwa ni jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Pia Serikali Kuu ya awamu ya sita, ilituongezea nguvu kwa kutupatia Halmashauri ya Wilaya fedha za Tozo jumla ya **Shilingi 20,000,000** kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania ambazo zitatumika kukuza miche ya Miti katika Shule **03** za Msingi (Mikocheni, Meka na Kigurusimba) na **03** za Sekondari (Tongani, Kipumbwi na Bushiri). Wastani wa Miche **72,000** inategemewa kuzalishwa na kusambazwa kwa Wadau mbalimbali kuanzia Mwezi Aprili 2025 kwa ajili ya kupandwa kwa lengo la kupunguza utegemezi wa Miti ya Asili.

### 9.3 Ufugaji wa nyuki

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Chini ya Ibara ya 69 (e) Kitengo kimejikita katika kutoa elimu ya ufugaji Nyuki kwa njia ya kisasa iliyotolewa kwa Vikundi vya Wafugaji wa Nyuki kwa Vikundi vya KAZI Pangani Magharibi, JIFUTE (Msaraza), MSETO II (Pangani Mashariki) na Ujirani Mwema (Mbulizaga) .
Kwa sasa, Wilaya ina Vikundi zaidi ya **42** vya ufugaji Nyuki na watu binafsi wapatao **14**. Uzalishaji wa asali umeongezeka kutoka wastani wa **kilo 1,288** hadi **1,388** za asali kwa kipindi hiki.

### 9.4 Wanyamapori

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Chini ya Ibara ya 69(c) Kitengo kiliendelea na usimamizi na uhifadhi wa Wanyamapori na kushughulikia Wanyama waharibifu kwenye mali za wananchi ikiwemo Tembo, Viboko, Mamba, Mbogo waliweza kudhibitiwa na kurudishwa hifadhini.

Aidha, Wanyama hawa walisababisha hasara kwa wananchi wapatao **54** wenye mashamba katika Vijiji vya Mtango, Mikinguni, Kwakibuyu, Mtonga na Langoni. Tathimini na hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya tathimini kwa mali za wahusika na kuwataarifu Wizara ya Maliasili ili wahanga hawa waweze kufanyiwa fidia kwa mujibu wa taratibu na kisheria.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa kipindi cha taarifa hii matatizo ya Wanyama pori sio makubwa japo baadhi ya wanyama kama Tembo waliingia kwenye mashamba ya wananchi wakitafuta maji, majani na uoto kipindi cha Januari Machi kukiwa na mazingira na kila kitu kikiwa katika hali nzuri na wanyama wakipata mahitaji yao katika mapori yao kusingelikuwa na athari za kimazingira.

## 9.5 MABADILIKO YA TABIA NCHI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Huu ni mfumo wa mabadiliko ya hali ya hewa yanayochukua muda mrefu au mfupi na kusababisha hali mbaya za hewa ama uchache wa hali inayohitajika au wingi wa hali

isiyohitajika na kusababisha madhara kwa jamii na nchi kwa ujumla. Kwa kipindi hiki kulikuwa na maeneo mengi kukumbwa na mafuriko kutokana na mvua zisizokuwa na mpangilio.

**Hatua zilizochukuliwa kukabiliana na Janga hili;**

i. Kuendelea kutoa elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kupitia kituo cha redio Pangani FM ambapo kila siku ya Ijumaa kuna kipindi kinachohusu utunzaji wa Mazingira kiitwacho **"NITUNZE NIKUTUNZE".**

ii. Kufanya kampeni ya upandaji Miti kupitia uzinduzi wa Wiki ya upandaji Miti (Arbor week) tarehe 01 hadi 07/04/2024

## 9.6 SHUGHULI ZA MADINI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Upo uwekezaji wa mashamba ya chumvi kwenye Kijiji cha Buyuni na Sange ambapo wawekezaji hawa wanasaidia kupatikana kwa ajira za muda pamoja na kusaidia jamii kama kwenye shughuli za Maendeleo Vijijini. Uzalishaji wa Chumvi haujaanza kutokana na Mvua zisizotabirika kuharibu ratiba ya utengenezaji Chumvi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kampuni ya (Nyati) Inatarajiwa kuanza Uzalishaji wa Madini baada ya kukamilisha taratibu za uchambuzi wa Athari za Mazingira na kufanya tathmini kwaajili ya kulipa fidia katika Kata za Bweni, Mwera, Tungamaa na Mikinguni.

## 10.0 MIUNDOMBINU, MAENDELEO YA VIJIJINI NA MIJINI

### 10.1 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri ya Wilaya ya Pangani kupitia Idara ya Miundombinu, Maendeleo Mijini na Vijijini ina sehemu **03** ambazo ni sehemu ya Ujenzi, Barabara na Maendeleo Mijini na Vijijini. Idara hii husimamia ujenzi na ukarabati wa majengo ya UMMA pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu wa masuala yote ya ujenzi wa majengo kwa watu binafsi, sambamba na hilo Idara kwa kushirikiana na Idara ya Afya na Idara ya Ardhi inaratibu utoaji wa vibali vya ujenzi na ukarabati.

### 10.2 MAJENGO MBALIMBALI KATIKA WILAYA.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani inatekeleza miradi ya ujenzi wa majengo mbalimbali katika Idara za Elimu Msingi, Elimu Sekondari, sekta ya Afya, sekta ya Kilimo na Uvuvi, kwenye kata na Vijijini. Miradi hiyo ya ujenzi/ukarabati wa majengo husimamiwa na Idara ya Miundombinu, Maendeleo Mijini na Vijijini.
Miradi mingi inatekelezwa kwa kutumia mafundi wa kawaida (Local Fundi) ambapo sehemu ya miradi hii hutegemea nguvu kazi za wananchi katika kuifanikisha.

**Mheshimiwa Mwenyekit**i, Aidha kumekuwa na changamoto za upatikanaji wa nguvu kazi kwa wakati au kukosekana kabisa na kupelekea baadhi ya miradi kutokukamilika kwa wakati au kutokukamilika kabisa kwasababu fedha zinazoletwa kutekeleza baadhi ya miradi hazitoshelezi kukamilisha miradi hiyo bila ya jamii kushiriki kikamilifu katika zoezi zima la uchangiaji wa nguvu kazi, kukosekana kwa fedha ya vifaa vya awali kama stoo ya muda, vyoo vya muda na fedha ya kupima vifaa pia baadhi ya malighafi zinazotumika katika ujenzi wa miundombinu hiyo zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya ghali na hata malighafi hizo zikipatikana zimekuwa zikichelewa kufika site kutokana na changamoto ya Miundombinu katika maeneo ya utekelezaji wa miradi. Changamoto hizi zimepelekea miradi kuchelewa kukamilika kwa wakati na wakati mwingine kutokamilika kabisa.

### 10.3 IDARA YA UTAWALA

#### 10.3.1 JENGO LA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI AWAMU YA TATU.

**Mheshimiwa Mweyekiti,** Ujenzi na umaliziaji wa jengo la halmashauri ya wilaya ya pangani awamu ya tatu (phase III) ni mradi unaotekelezwa kwa mfumo wa Mkandarasi Associated Investment and Services Limited. Na kusimamiwa na mshauri y&p. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa 30$^{th}$ November 2021 kati ya halmashauri ya wilaya ya Pangani (employer) na Mkandarasi Associated Investment and Services Limited. (The constructor) wakati ujenzi halisi ulianza 14$^{th}$ December 2021, baada ya kukabidhiwa eneo la ujenzi on 30$^{th}$ November 2021.Mradi huu unahusisha kazi za ujenzi na umalizaiji wa majengo yafuatayo;

- Jengo kuu lenye ghorofa moja (Main Building)
- Mazingira ya Nje (Landscaping)
- Uzio (Fence Wall)

### 10.3.2 MAENDELEO YA MRADI

Hatua iliyofikiwa mpaka sasa ni asilimia 55% ya utekelezaji wa Mradi kwa ujumla.

#### I. SAKAFU YA CHINI (GROUND FLOOR PLAN)

- Mihimili (frame structure) imekamilika column na beam umekamilika
- Ujenzi wa tofari katika sakafu ya chini imekamilika.
- Upigaji wa plasta njee na ndani imekamilika
- Ujezi wa ngazi mterezo ramp umekamilika
- Skimimg ya jengo upande wa ndani umekamilika kwa 80%
- Uwekaji wa marumaru sakafu ya chini umekamilika kwa 70%
- 'First fix' ya kazi za Umeme umekamilika
- 'First fix' ya kazi za 'Plumbing' umekamilika
- 'First fix' ya kazi za TEHAMA umekamilika

Katika ujenzi wa jengo kuu lenye ghorofa moja (main building)

Kazi ambazo bado hazijakamilika mpaka sasa kwa asilimia mia moja (100%) Jengo kuu lenye ghorofa moja (main building) Gorofa moja ni kama zifuatazo: -ndogondogo (Building services) ili kukamilisha kazi zifuatazo;

- Ukamilishaji wa ufungaji wa huduma za Viyoyozi haujakamilika
- Ukamilishaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA haujakamilika
- Ukamilishaji na ufungaji wa vifaa vya Umeme haujakamilika
- Umaliziaji wa upakaji wa rangi ya nje na ndani mkono wa pili na wa tatu (second and final coat) haujakamilika
- Kazi za nje: kujenga mifereji ya kusafirisha maji, kuweka 'kerbstones' haujakamilika
- Kuweka kazi ya 'Landscape' ('paving' na upandaji Maua/Majani) haujakamilika
- Ukamilishaji na ufungaji wa vifaa vya bomba awamu ya pili upande chooni na jikoni
- Kukamilisha Skimimg ya jengo upande wa ndani kwa 20% haujakamilika
- Kukamilisha Uwekaji wa marumaru sakafu ya chini kwa 30% haujakamilika
- Uwekaji wa grill za madirisha na madirisha ya allumiumn bado haujakamilika
- Uwekaji wa flame na shata za milango bado haujakamilika

#### II. SAKAFU YA KWANZA (FIRST FLOOR PLAN)

Katika ujenzi wa jengo kuu lenye ghorofa moja (main building) Kazi ambazo zimeshakamilika mpaka sasa kwa asilimia mia moja (100%) Jengo kuu lenye ghorofa moja (main building) Gorofa moja ni kama zifuatazo

- Mihimili (frame structure) imekamilika column na beam.
- Ujenzi wa ngazi mterezo ramp umekamilika
- 'First fix' ya kazi za Umeme umekamilika
- 'First fix' ya kazi za 'Plumbing' umekamilika
- 'First fix' ya kazi za TEHAMA umekamililka

- ‘Ujenzi wa concrete gutter umekamilika

Katika ujenzi wa jengo kuu lenye ghorofa moja (main building) Kazi ambazo bado hazijakamilika mpaka sasa kwa asilimia mia moja (100%) Jengo kuu lenye ghorofa moja (main building) Gorofa moja ni kama zifuatazo: -ndogondogo (Building services) ili kukamilisha kazi zifuatazo;

- Ukamilishaji wa ufungaji wa huduma za Viyoyozi haujakamilika
- Ukamilishaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA haujakamilika
- Ukamilishaji na ufungaji wa vifaa vya Umeme haujakamilika
- Umaliziaji wa upakaji wa rangi ya nje na ndani mkono wa pili na wa tatu (second and final coat) haujakamilika
- Upigaji wa plasta njee na ndani haujakamilika
- Ukamilishaji na ufungaji wa vifaa vya bomba awamu ya pili upande chooni
- Kukamilisha Skimimg ya jengo upande wa ndani kwa haujakamilika
- Kukamilisha Uwekaji wa marumaru sakafu ya juu haujakamilika
- Uwekaji wa ‘dari (ceiling board)
- bao haujakamilika
- Kupaua na kuezeka haujakamilika
- Kumwage zege baadhi ya roof slab haujakamilika
- Uwekaji wa grill za madirisha na madirisha ya allumiumn bado haujakamilika
- Uwekaji wa flame na shata za milango bado haujakamilika

## 10.3 SEKTA YA ELIMU.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Idara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Idara za Elimu Sekondari na Elimu Msingi husimamia ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya majengo mbalimbali yaliyopo kwenye Shule mbalimbali ndani ya wilaya ya Pangani ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

### 10.3.1 ELIMU SEKONDARI.

- Kusimamia ujenzi wa shule mpya ya kidato cha I-VII katika kata ya Pangani Mashariki
- Kusimamia ujenzi wa nyumba ya walimu vyumba viwili vya kulala (2 in 1) katika shule ya sekondari Masaika.
- Kusimamia umaliziaji wa mabweni mawili shule ya sekondari Funguni.

#### 10.3.1.1 HALI HALISI YA UTEKELEZAJI.

**Shule ya Sekondari Funguni.**

- Umaliziaji wa maweni mawili katika shule hii unaendelea katika hatua za mwisho.
- Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari ya Pangani Mashariki kata ya Pangani Mashariki Wilaya ya Pangani unajumuisha ujenzi wa Majengo yafuatayo: -

i. Jengo la Utawala
ii. Jengo la Madarasa Vyumba viwili na Ofisi (Block Mbili)
iii. Jengo la Madarasa Vyumba viwili bila Ofisi (Block Mbili)

iv. Jengo la Komputa (ICT Block)
v. Jengo la Maktaba (Library Block)
vi. Jengo la Maabara ya Kemia na Bailojia
vii. Jengo la Maabara ya Fizikia
viii. Matundu ya Vyoo vya Wavulana (Matundu 5)
ix. Matundu ya Vyoo vya Wasichana (Matundu 6)
x. Tenki la Kutunza Maji la Ardhini

Maendeleo ya mradi kwa asilimia za utekelezaji yanaonekana kwenye Jedwali la chini;

**Jedwali Na. 1 Miradi ya maendeleo kwa asilimia ya utekelezaji**

| AINA YA JENGO | Asilimia ya Utekelezaji (%) | Hatua ya ujenzi |
|---|---|---|
| JENGO LA UTAWALA | 55 | upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |
| MADARASA 2 NA OFISI (1 BLOCKS) | 65 | upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |
| MADARASA 2 NA OFISI (1 BLOCKS) | 65 | upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |
| MADARASA 2 BILA OFISI - 01 BLOCK | 55 | upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |
| MADARASA 2 BILA OFISI - 01 BLOCK | 65 | upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |
| JENGO LA KOMPyUTA | 40 | Maandalizi kusuka kenchi yanaendelea |
| JENGO LA MAKTABA | 65 | upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |
| JENGO LA MAABRA YA KEMIA NA BIOLOJIA | 55 | Ujenzi wa meza na upigaji wa plasta nje na ndani unaendelea |

| | | |
|---|---|---|
| JENGO LA FIZIKIA | 40 | Maandalizi kusuka kenchi yanaendelea na kupiga plasta yanaendelea |
| VYOO VYA WASICHANA NA KICHOMEA TAKA | 50 | Ujenzi wa mashimo ya maji taka yanaendelea |
| VYOO VYA WAVULANA TENKI LA MAJI | 50 | Ujenzi wa mashimo ya maji taka yanaendelea |

**Shule ya Sekondari Masaika.**

- Ujenzi wa nyumba ya walimu vyumba viwili vya kulala (2 in 1) katika shule ya sekondari Masaika uko katika hatua ya kupiga bati.

## 10.4 ELIMU MSINGI

- kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu 6 ya vyoo katika shule ya msingi mbulizaga
- kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi kimanga.
- kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi boza.
- kusimamia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi madanga.

**Jedwali na. 2 Hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo**

| Na. | Aina ya Ujenzi/Mradi | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na matundu 6 ya vyoo katika shule ya msingi mbulizaga | Ujenzi umekamilika |
| 2 | Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi kimanga. | Ujenzi umekamilika |
| 3 | Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi boza. | Ujenzi umekamilika |
| 4 | Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ya awali na matundu sita ya vyoo katika shule ya msingi madanga. | Ujenzi umekamilika |

## 10.5 SEKTA YA AFYA

### 10.5.1 UJENZI WA ZAHANATI YA MWEMBENI.

- Kufanya makisio ya majengo mawili (OPD na MATERNITY) katika zahanati ya mwembeni.

- Kusimamia ujenzi wa majengo mawili (OPD na MATERNITY) katika zahanati ya mwembeni.

### 10.5.2 UJENZI WA ZAHANATI YA MIKINGUNI.

- Kufanya makisio ya majengo mawili (OPD na MATERNITY) katika zahanati ya mikinguni.
- Kusimamia ujenzi wa majengo mawili (OPD na MATERNITY) katika zahanati ya mwembeni

### 10.5.3 UMALIZIAJI WA ZAHANATI YA BUYUNI.

- Kuandaa makisio ya Umaliziaji wa jengo la zahanati ya buyuni.
- Kusimamia umaliziaji wa jengo.

### 10.5.4 UMALIZIAJI WA ZAHANATI YA MSEKO.

- Kusimamia ujenzi wa matundu ya vyoo Pamoja na zahanati
- Kuandaa makisio ya Umaliziaji wa jengo la zahanati ya Mseko.

### 10.5.5 UTEKELEZAJI WA MRADI WA SRWSSP

- Kusimamia utekelezaji wa mradi wa SRWSSP katika zahanati ya Masaika, Bushiri, Kimanga na Kipumbwi (ujenzi wa matundu matatu ya vyoo vikijumuisha choo cha walemavu, mnara wa maji, miundombinu ya kunawia mikono, kukarabati vyoo vya watumishi Pamoja na ujenzi wa kichomea taka, shimo la majivu na shimo la kutupia kondo la nyuma).

- Kuandaa makisio ya kutekeleza miradi hii ya mpango wa maji safi yaani SRWSSP

**Jedwali na.3 Hali halisi ya utekelezaji wa miradi katika Sekta ya Afya**

| Na. | Aina ya Ujenzi/Mradi | Hatua ya utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Zahanati ya Mwembeni | Ujenzi wa top kozi |
| 2 | Ujenzi wa Zahanati ya Mikinguni | ujenzi wa linta |
| 3 | Umaliziaji wa jengo la zahanati ya buyuni. | Hatua ya umaliziaji |
| 4 | Umaliziaji wa jengo la zahanati ya Mseko | Jengo liko kwenye ukamilishaji, ujenzi wa vyoo uko umaliziaji |
| 5 | Kusimamia utekelezaji wa mradi wa srwss katika zahanati ya Masaika, Bushiri, Kimanga na Kipumbwi (ujenzi wa matundu matatu ya vyoo vikijumuisha choo cha walemavu, mnara wa maji, miundombinu ya kunawia mikono, kukarabati vyoo vya watumishi Pamoja na ujenzi wa kichomea taka, shimo la majivu na shimo la kutupia kondo la nyuma. | Mradi umekamilika |
| | Kusimamia utekelezaji wa mradi wa srwss katika shule ya msingi Tugamaa na Mtonga (ujenzi wa matundu vyoo vikijumuisha choo cha walemavu na | Mradi umekamilika |

| | | |
|---|---|---|
| | chumba maalum kwa vyoo vya wasichana, mnara wa maji, miundombinu ya kunawia mikono.) | |

**10.6 VIBALI VYA UJENZI.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Idara ya Miundombinu maendeleo mijini a vijijini kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi pamoja na Afya (W) inaendelea kuratibu utoaji wa vibali vya ujenzi, kamati maalumu ya watu 5 iliundwa kwa mujibu wa sheria kwaajili ya kuratibu zoezi la kupitia ramani (scrutinization) mbalimbali pamoja na kuhakiki umiliki wa viwanja/maeneo husika kabla ya kutoa kibali husika, Aidha kwa kipindi cha robo ya pili vibali vya ujenzi vyenye thamani ya **Shilingi 4,745,108.00** vimetolewa sawasawa na asilimia **158**%.

**10.7 KODI ZA MAJENGO (PROPERTY TAX) NA PANGO LA ARDHI (LAND RENT).**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Idara ya Miundombinu Maendeleo Mijini na Vijijini inaendelea kuratibu zoezi la uoreshaji wa kazidata wamilika wa majengo yote katika halmashauri ya wilaya ya pangani ili kuwezesha halmashauri kupata mapatao stahiki. Mpaka sasa halmashauri imefaikiwa kupokea takriani **Shilingi 11,662,654.00** ambazo ni gawio la 20% kwa mujibu wa mwongozo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Aidha mpaka sasa halmashauri haijapokea gawio la asilimia ishirini la kodi ya ardhi hivyo kupelekea kuathiri mapato. jitihada zinaendelea kuhakikisha halmashauri inanufaika na hili kwa mujibu wa mwongozo.

**10.8 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

- Upungufu wa fedha za utekelezaji wa miradi ya ujenzi toka Serikali kuu hasa ujenzi wa Mabweni na vyoo kwani fedha zinazoletwa haziendani na bei halisi ya malighafi/vifaa vinavyohitajika kukamilisha ujenzi husika.
- Upungufu wa vifaa vya usafiri vya kuwezesha wataalamu wa ujenzi kufika maeneo ya ujenzi.
- Mwitikio mdogo wa wananchi katika kushiriki/kuchangia ujenzi wa miradi inayowazunguka.
- Ukosefu wa maji mara kwa mara katika maeneo mengi ya Ujenzi.
- Kuchelewa kwa vifaa vya ujenzi pindi vinapoagizwa.
- Baadhi ya miradi kuwa mbali na maeneo yanayopatikana/yanapotoka malighafi/vifaa vya ujenzi.

**10.8.1 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Idara imekuwa na changamoto nyingine kama ifuatavyo; -

- **Watumishi.**

Idara inaupungufu wa watumishi akiwepo Mkuu wa Idara (DE), Mhandisi Mitambo, Mafundi sanifu ujenzi, maji, Mitambo, pamoja na wahudumu wa ofisi, hivyo kupelekea utendaji wa

kazi kuwa na changamoto nyingi hasa ukizingatia miradi yetu hutekelezwa kwa kutumia Mafundi wa Kawaida (Local Fundi's) ambao huhitaji usimamizi wa karibu sana na hivyo kuwepo ugumu katika kufanya kazi nyinginezo.

- **Usafiri na Vitendea kazi.**

Idara ya ujenzi kwasasa inazo pikipiki mbili ambazo ni za kuazima, pikipiki hizo husaidia kufika mara chache kwenye miradi iliyopo maeneo ya karibu inayoendelea kutekelezwa ndani ya Wilaya. Hata hivyo usafiri huo hautoshelezi hasa ukizingatia tunayo miradi mingi ambayo inatakiwa kukaguliwa na kusimamiwa kila mara. Idara imekuwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile Computer, na mashine ya kudurufu (photocopier). Kwa sasa idara inayo Printer na Computer moja tu. hivyo kulazimisha baadhi ya watumishi wa idara kutumia computer zao binafsi.

### 10.8.2 MIKAKATI YA UTATUZI WA BAADHI YA CHANGAMOTO.

- ✓ Kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii kutoa elimu juu ya umuhimu wa wananchi kushiriki katika Ujenzi/utekelezaji wa Miradi hasa miradi inayotekelezwa kwa kutumia mafundi wa kawaida (Local Fundi)
- ✓ Sekta zote zenye miradi zishirikiane na Vijiji/Kata husika katika kutatua changamoto zilizopo kwenye uwezo wao kama vile changamoto ya ukosefu wa maji ya ujenzi, mchanga, mawe na kokoto kwani malighafi hizi zinapatikana kwenye maeneo yanayozunguka miradi mingi.
- ✓ Idara pia imekuwa ikiomba usafiri kutoka idara husika ambapo sio mara zote maombi hayo yametekelezeka.
- ✓ Idara ikishirikiana na idara ya mipango katika kufanya matengenezo ya gari mojawapo ili kuwezesha usimamizi wa miradi.

## 11.0 SEKTA YA TEHAMA

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kitengo hiki kinatekeleza **Ibara ya 102(L):** ambayo inaelekeza; Kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika Uchumi wa Kidijitali (digital economy) hususani Serikali mtandao, Miundombinu ya TEHAMA katika Nyanja zote za Uchumi na Ulinzi wa Mitandao.

### Utekelezaji:

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa majukumu ni kama ifuatavyo;-

### A) Kusimamia Email za Serikali (Government Mail System)

Kitengo cha Tehama kwa Kushirikiana na Idara na Vitengo kinasimamia Email zote za Serikali za Idara na Vitengo vya Halmashauri.

### Matokeo

Kuongezeka kwa Utunzaji wa nyaraka za Siri za Serikali.

**B) Kusimamia mfumo ya FFARS**

Tehama kwa kushirikiana na Idara ya Mipango na Kitengo cha Fedha na Uhasibu imesimamia Mfumo wa FFARS ambao unatumiwa na Vituo **21** vya kutolea Huduma za Afya, Vijiji **33**, Shule **09** za Sekondari na Shule **34** za Msingi katika Halmashauri kwa ajili ya kufanya matumizi kwa kupitia mfumo wa FFARS.

**Matokeo**

Kurahisisha matumizi ya upokeaji, utoaji na matumizi ya fedha za Serikali

**C)Kusimamia mfumo wa PLANREP**

Kitengo cha Tehama kwa kushirikiana na Idara na Vitengo vya Halmashauri kimesimamia mfumo wa PLANREP wakati wa uandaaji Bajeti ya mwaka wa Fedha 2024/2025

**Matokeo**
Kurahisisha kupanga bajeti, kuandaa mipango na kutoa taarifa ya yale yatakayokuwa yametekelezwa katika eneo husika.

**E) Kusimamia mfumo wa TEN PERCENT LOAN MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM(TPLMIS)**

Kitengo cha Tehama Kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii kimesimamia mfumo wa Utoaji wa Mikopo wa Asilimia kumi (10%) Halmashauri.

**Matokeo**

Kuongezeka kwa ufanisi wa utoaji wa mikopo kwa makundi ya wanawake, walemavu na vijana

**F) KUSIMAMIA MFUMO WA KUTOA VYETI VYA CHANJO YA UVIKO19**

Kitengo cha TEHAMA kwa kushirikiana na Ofisi ya DMO inaendelea kusajili watumiaji wa Mfumo wa kutoa Vyeti vya Chanjo ya **UVIKO 19**, Hospitali ya Wilaya ya Pangani, Vituo vya kutolea huduma za Afya, na Zahanati. hivyo basi ambao wamechanjwa watapata Vyeti vya Chanjo vya Kieletroniki kwa njia ya simu na barua pepe.

**G) Kusimamia Mfumo wa SELFORM**

Kitengo cha TEHAMA kwa kushirikiana na Idara ya Elimu Sekondari kinaendelea kusimamia mfumo wa Selform wa ujazaji wa uchaguzi wa kujiunga na mwaka wa masomo 2024 kwa Shule za kidato cha tano na sita na vyuo vya kati kwa Wanafunzi waliohitimu kidato cha nne Mwaka 2023.

## H) KUSIMAMIA MFUMO WA SELECTION

Kitengo cha Tehama kwa kushirikiana na Idara ya Elimu Sekondari na Idara ya Elimu Msingi na Wataalamu wa Tamisemi kimesimamia mfumo wa Kuchagua Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa Mwaka wa Masomo 2024.

## I) KUSIMAMIA MFUMO WA SCHOOL INFORMATION SYSTEM (SIS)

Kitengo cha TEHAMA kimeweza kusimamia Mfumo wa Taarifa za Walimu na Wanafunzi Mashuleni.

## J) KUSIMAMIA MFUMO WA PREM

Kitengo cha Tehama kwa kushirikiana na Idara ya Elimu Msingi kimesimamia mfumo wa PREM kwaajili ya Kuhamisha Wanafunzi wa shule za msingi kutoka shule moja kwenda shule nyingine, Kutoa namba ya usajili wa Mwanafunzi, kutunza kumbukumbu za maendeleo ya Mwanafunzi kwa kujaza matokea yake.

## K) KUSIMAMIA MFUMO WA PREMS

Kitengo cha Tehama kwa kushirikiana na Idara ya Elimu Sekondari, imesimamia mfumo wa PREM kwa ajili ya Kuhamisha wanafunzi wa shule za Sekondari kutoka shule moja kwenda shule nyingine, Kutoa namba ya usajili wa Mwanafunzi.

## L) KUSIMAMIA MTANDAO WA NDANI WA HALMASHAURI.

Kitengo cha TEHAMA kimeweza kusimamia mtandao wa ndani wa Halmashauri (Local Area Nertwork) na kutatua changamoto mbalimbali.

## M) KUSIMAMIA MFUMO WA GOTHOMIS

Kitengo cha TEHAMA Kinaendelea kusimamia mfumo wa Kutoa Huduma kwenye Hospitali ya Wilaya pamoja na Zahanati na Vituo vya kutolea Huduma za Afya na Pia kushirikiana na Mganga Mkuu kuhakikisha Zahanati ambazo bado hazijafungiwa mfumo wa GoT-HoMIS zinafungiwa Mfumo

## N) Kusimamia Mfumo wa kieletronikia wa mapato (LGRCIS) pamoja na vifaa vinavyotumika kwenye ukusanyaji wa mapato ‘POS’

Kitengo cha TEHAMA kinasimamia mfumo wa kieletroniki wa mapato shughuli za usimamizi zilizofanywa na kitengo cha TEHAMA ni pamoja na: -

- Kutoa elimu kwa watumiaji wa POS juu ya matumizi ya Vifaa vya ukusanyaji Mapato,

Kitengo cha TEHAMA kimefanikiwa kutoa elimu ya matumizi ya Vifaa vya kukusanyia Mapato katika vijiji vilivyopo katika Halmashauri ya wilaya ya Pangani, kwa kushirikiana na Idara ya Fedha na

Uhasibu. Hii imesaidia katika kuongeza uelewa wa jinsi ya ukusanyaji wa mapato na namna ya kutunza vifaa hivyo kwani elimu hiyo iliweza kutolewa katika maeneo yao ya utendaji kazi.

- Kusimamia Miundombinu ya Mfumo wa Mapato (LGRCIS)

Kitengo pia kimeweza kusimamia Miundombinu yote inayoizunguka mfumo ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na wataalamu kutoka OR-Tamisemi ili kuhakikisha mfumo unafanya kazi kwa muda wote wa kazi na kwa ufanisi mkubwa.

**O) Kusimamia mfumo wa MUSE**

Kitengo cha TEHAMA kwa Kushirikiana na Idara ya Fedha na Uhasibu kinatatua changamoto kwenye mfumo wa MUSE kwa kushirikiana na Wataalamu wa Tamisemi**.**

**p) Kusimamia mfumo wa ununuzi wa NeST**

Mfumo wa kuwezesha usajili wa kielektroniki, zabuni za kielektroniki, usimamizi wa mikataba ya kielektroniki, malipo ya kielektroniki, katalogi na mnada wa kielektroniki.

**Matokeo**

Inasaidia michakato ya ununuzi wa Bidhaa, Kazi, Ushauri, Usio wa Ushauri na Utupaji wa mali. Mfumo huu unasaidia taratibu mbalimbali za manunuzi ya umma ikiwa ni pamoja na usajili wa watumiaji, taarifa za zabuni, utayarishaji na uwasilishaji zabuni, tathmini ya zabuni kwa njia ya mtandao, utoaji wa mikataba, uundaji na usimamizi wa katalogi, uundaji na usimamizi wa mikataba ya mifumo na minada na malipo.

**Q) KUSIMAMIA MFUMO WA CMG** (**Community Microfinance Groups)**

Mfumo wa Benki Kuu ya Tanzania wa usajili wa Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha

**Matokeo**

Kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za usajili, usimamizi na za kiutendaji zinazohusiana na usimamizi, utoaji mikopo, ruzuku na dhamana ya mikopo iliyotolewa kwenye Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**R) KUSIMAMIA MFUMO WA MUKI**

Mfumo wa Ujifunzaji Kielekroniki Kwa ajili ya Waajiliwa Wapya wa Halmashauri ya wilaya ya Pangani.

**S) KUSIMAMIA MFUMO WA ASC** Sensa Elimu Msingi

## 12.0 KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kitengo cha Mawasiliano Serikalini imeendelea kutekeleza shughuli zifuatazo;-

i. Kuandika habari za utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, kwa njia ya Tovuti, twitter, Facebook na Instagram
ii. Kuutarifu umma kuhusu masuala mbalimbali kama vile mapokezi na matumizi ya fedha kutoka serikali kuu, na maelekezo ya matumizi yake na ushahidi wa picha za utekelezaji wake .
iii. Kuhuisha tovuti ya Halmashauri kwa kuweka habari na taarifa mbalimbali zinazohusiana na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Halmashauri.
iv. Kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kwa waandishi wa habari pamoja na wananchi wanaouliza maswali kupitia mitandao ya Halmashauri ikiwemo facebook, twitter na Instagram.
v. Kuhabarisha wananchi kuhusu matukio mbalimbali ya halmashauri kupitia tovuti rasmi ya Halmashauri ya Wilaya ya Pangani Pamoja na mitandao ya kijamii.
vi. Kuongeza wigo wa uhabarishaji na kuendelea kufikisha taarifa mbalimbali kwa wananchi kwa kuanzisha **YouTube Channel** inayojulikana kwa jina la **Pangani DC.**

### CHANGAMOTO

Upungufu wa Watumishi wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali ikama ni Watumishi watatu (**03**) na kwa sasa kitengo kina mtumishi mmoja (**01**) hivyo kua na upungufu wa Watumishi wawili (**02**).

## 13.0 SEKTA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sekta ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia kitengo chake imetekeleza shughuli mbalimbali za Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ifuatavyo;

**UTAMADUNI**

i. **Ibara 188(i**) – Kuboresha utekelezaji wa mipango ya maandalizi na ushiriki wa wananchi katika sherehe za kitaifa, kidini, kiserikali na kijamii.

**Utekelezaji,**

a) Kuratibu maadhimsho ya siku ya kumbukizi ya mashujaa kwa ngazi ya Wilaya tarehe 25 Julai 2024 katika maeneo ya soko kuu la Pangana(Pangani Magharibi).
b) Kuwezesha maafisa kushiriki tamasha la tatu la utamaduni kitaifa lililofanyika tarehe 20-23 Septemba, 2024 Mkoani Ruvuma.
c) Kuratibu zoezi la sherehe za miaka 63 ya uhuru wa Tanzania bara Kiwilaya tarehe 9 Disemba 2024 katika viwanja vya Boma. Katika sherehe izo wananchi na watumishi waliweza kushiriki kwa zoezi la kupanda miti na kufanya usafi wa mazingira.
d) Kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa sanaa juu ya fursa za upatikanaji wa mikopo kutoka taasisi ya mfuko wa utamaduni na sanaa (TACAF) kata ya Masaika na Bushiri.
e) Halmashauri kuanzia mwezi Julai hadi Disemba, 2024 imekusanya Mapato ya kiasi cha **Shilingi 8,849,307.00** sawa na asilimia **67%** kupitia utoaji wa Vibali vya Sherehe na Matangazo na pia uhamasishajii wa Wanajamii katika utunzaji na uendelezaji wa mali kale na tamaduni ambazo zinapatikana ili kuendeleza tunu za historia ya nchi yetu na Wilaya ya Pangani kwa ujumla kwa faida ya Vizazi vijavyo.

**SANAA**

ii. **Ibara ya 188 (e);** Kuendelea kuimarisha mfumo wa kuibua vipaji vya wasanii na kuwatunza na kuwaenzi wasanii wakongwe waliohai na waliofariki

**Utekelezaji,** Kutoa elimu ya usajili wa Wasanii na kazi zao kupitia mfumo wa kidigital unaitwa AMIS ambao uko chini ya Balaza la Sanaa la Taifa (BASATA). Hii itamwezesha Msanii wa kazi za Sanaa kuweza kutambulika, kusajili kazi zake na kujisajili yeye binafsi, kikundi au bendi. Hii pia itasaidia kulinda hati miliki za Msanii. Kupitia maandalizi ya sherehe za miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania bara kitengo kiliweza kuratibu mashindano ya Sanaa za uandishi wa Insha kwa shule za Msingi na Sekondari ambapo washindi walipewa tuzo (Zawadi) siku ya kilele cha sherehe za miaka 63 ya uhuru wa Tanzania bara tarehe 09 Disemba 2024.

**MICHEZO**

iii. **Ibara 188(g) -** Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa michezo katika skuli, vikosi, wizara, mitaa na jamii kwa ujumla kwa kushirikiana na vyama husika.

**Utekelezaji,**

a) Kuratibu bonanza la michezo kati ya watumishi wa Halmashauli ya Wilaya ya Pangani dhidi ya watumishi wa Halmashauri ya Lushoto tarehe 27/07/2024.

b) Kufuatilia utekelezaji wa ratiba za michezo kwa shule tatu za msingi (Shule ya msingi Funguni, Pangani na Boza) na Shule moja ya Sekondari (Funguni sekondari).
c) Kufanikisha watumishi kushiriki bonanza la michezo lililoandaliwa na uongozi wa mkoa tarehe 28/09/2024.
d) Kushiriki kikao kazi cha tathimini ya michezo cha maafisa na walimu wa michezo tarehe 16/08/2024 Mkoani Tanga.
e) Kuratibu bonanza la michezo la climate change marathon kwa kushirikiana na taasisi isio ya kiserikali ijulkanayo kama tree of hope, bonanza lilihusisha michezo mbalimbali kama mbio za kilometa 5,10 na 21 na mbio za kukimbiza kuku, mpira wa miguu, mpira wa pete/Netball na mchezo wa Pool table.
f) Kuratibu uchaguzi wa viongozi wa chama cha riadha cha Wilaya tarehe 25 Octoba, 2024 na kuwasilisha majina Mkoani.

## 14.0 KITENGO CHA UCHAGUZI

**Mheshimiwa mwenyekiti,** Halmashauri ya Wilaya ya Pangani imetekeleza zoezi la Uchaguzi wa serikali za Mitaa lililofanyika tarehe 27/11/2024 katika Kata 14, Vijiji 33 na Viongoji 96. Vyama vya Siasa vilivyoshiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 ni CCM, CHADEMA, CUF, ACT- Wazalendo na NCCR-Mageuzi.

### 14.1 UTEUZI WA WAGOMBEA WALIOSHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ilianza na zoezi la Ugawaji na Urejeshwaji wa fomu za wagombea katika Ofisi za Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Vijiji kuanzia tarehe 26/10/2024 hadi 01/11/2024 na uteuzi ulifanyika tarehe 08/11/2024, Wagombea walioteuliwa walikuwa kama wafuatao;

**Jedwali na.1 Mwenyekiti wa Kijiji**

| CHAMA | IDADI YA WAGOMBEA |
|---|---|
| CCM | 33 |
| ACT – WAZALENDO | 10 |
| CHADEMA | 8 |
| CUF | 8 |
| NCCR MAGEUZI | 3 |
| **JUMLA** | **62** |

**Jedwali na.2 Mwenyekiti wa Kitongoji**

| CHAMA | IDADI YA WAGOMBEA |
|---|---|
| CCM | 96 |
| ACT – WAZALENDO | 17 |
| CHADEMA | 25 |
| CUF | 17 |

| | |
|---|---|
| NCCR MAGEUZI | 2 |
| **JUMLA** | **157** |

**Jedwali na.3 Wajumbe Mchanganyiko**

| **CHAMA** | **IDADI YA WAGOMBEA** |
|---|---|
| CCM | 433 |
| ACT – WAZALENDO | 49 |
| CHADEMA | 95 |
| CUF | 60 |
| NCCR MAGEUZI | 1 |
| **JUMLA** | **638** |

**Jedwali na.4 Wajumbe Kundi la Wanawake**

| **CHAMA** | **IDADI YA WAGOMBEA** |
|---|---|
| CCM | 264 |
| ACT – WAZALENDO | 13 |
| CHADEMA | 38 |
| CUF | 30 |
| NCCR MAGEUZI | 0 |
| **JUMLA** | **345** |

### 4.2 MATOKEO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024

**Mheshimiwa mwenyekiti**, Halmashauri ya Wilaya ya Pangani katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa **2024**, kulikuwa na vituo vya kupigia kura **118** venye Jumla ya wapiga kura **48,516** na Wananchi waliojitokeza kupiga kura ni **45,403** sawa na **93.6%** na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo; -

- Wenyeviti wa Vijiji -
  Chama cha Mapinduzi **– Vijiji 33 sawa na 100%**
- Wenyeviti wa Vitongoji –
  Chama cha Mapinduzi - **Vitongoji 96 sawa na 100%**
- Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji Kundi Mchanganyiko
  Chama cha Mapinduzi – **433 – sawa na 100%**
- Wajumbe wa Halmshauri ya Kijiji kundi la Wanawake
  Chama cha Mapinduzi – **264 sawa na 100 %**

### 4.3 CHANGAMOTO

**Mheshimiwa mwenyekiti,** Wananchi wengi walijittokeza kaika kujiandikisha katika Orodha ya Wapiga kura na siku ya kupiga kura.

### 4.3.1 UTATUZI WA CHANGAMOTO

**Mheshimiwa mwenyekiti**, Halmashauri ilitulazimu kuongeza vituo vipya **22**, kwenye maeneo yenye msongamano mkubwa watu na kuongeza askari wawili wawili kwa kila kituo.

# UTEKELEZAJI WA ILANI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI DISEMBA, 2024 KUPITIA SEKTA MBALIMBALI ZA SERIKALI KUU NDANI YA WILAYA YA PANGANI

## 14.0 SEKTA YA MAJI

Lengo la Wilaya ni kuona kunakuwa na Usalama wa Maji na kwamba huduma ya Maji Safi na Salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia Zaidi ya asilimia **85** ya Wakazi wa Vijijini na zaidi ya asilimia **95** kwa Mijini ifikapo 2025

### 14.1 MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA (TANGA UWASA)

#### 14.1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mamlaka ya majisafi na usafi wa Mazingira Tanga (Tanga UWASA) ilianzishwa rasmi tarehe 1, Julai 1998 kwa lengo la kutoa huduma za usambazaji wa majisafi na uondoshaji wa majitaka kwa wakazi wa Mjini Tanga. Mwaka 2019 kufuatia mabadiliko ya sheria, mipaka ya Tanga UWASA katika utoaji huduma ilitanuliwa na kujumuisha Kata sita (6) zilizopo Mjini Muheza na kata nne (4) za Mjini Pangani (Pangani Magharibi, Pangani Mashariki, Kimang'a na Madanga).

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Usimamizi wa huduma chini ya Tanga UWASA katika Mji wa Pangani ulianza rasmi Tarehe 06.09.2019 kufuatia tamko la Mhe. Waziri wa maji la kuifuta Mamlaka ya Maji ya Pangani (PUWASA) iliyokuwepo tangu Tarehe 30, Aprili 2004.

#### 14.1.2 Huduma ya Majisafi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, eneo la huduma kwa upande wa Pangani lina wakazi wapatao 20,780 ambapo mahitaji ya maji ni wastani wa lita 2,050,000 kwa siku. Chanzo cha maji kwa eneo la Pangani kwa sasa ni visima 6 ambavyo kufuatia mabadiliko ya tabia nchi, visima vitatu (3) ndivyo vinavyofanya kazi na vina uwezo wa kuzalisha maji wastani wa lita 950,000 kwa siku. Upatikanaji wa maji ni wastani wa saa 6 kwa siku na yanapatikana kwa 70% ya wakazi wa eneo la huduma.

#### 14.1.3 Huduma ya Uondoshaji wa Majitaka

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Huduma ya uondoshaji wa majitaka katika Mji wa Pangani hufanywa kwa kutumia gari za kunyonya majitaka pamoja na vyoo ambavyo vingi siyo rafiki wa mazingira. Aidha, Mamlaka imesajili jumla ya magari 12 ya kunyonya majitaka kutoka kwa wakazi wa maeneo ya huduma ambapo magari matatu yanamilikiwa na Tanga UWASA yenyewe ikiwa na lengo la kuleta gari moja wapo kukaa na kuhudumia wakazi wa Mjini Pangani na maeneo jirani baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu uliopo katika hatua za mwishoni.

### 14.1.4 Miradi kuongeza upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Tanga UWASA imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuboresha huduma za Majisafi na Uondoshaji wa Majitaka kwa wakazi waliopo katika maeneo ya huduma ili kutekeleza agizo la Ilani ya Chama Tawala (kufikia 95% kwa huduma ya majisafi kwa wakazi waliopo Mijini ifikapo 2025) lakini pia kufikia malengo ya kitaifa ikiwamo kufikia 30% ya wakazi kwa huduma ya uondoshaji wa Majitaka ifikapo 2030. Miradi hiyo ni pamoja na

| Sn | Jina la Mradi | Thamani | Pesa zilizotolewa | Hatua (%) iliyofikiwa | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Uendelezaji na ukarabati wa miundombinu ya maji Mjini Pangani (15km) | TZS 1,000,000,000 | TZS 574,502,255 | 75 | Jumla ya 11,400m zimeshalazwa,<br>Kazi ya uchimbaji kisima 1 imekamilika |
| 2 | Ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kata za Kimang'a na Madanga (15km) | TZS 554,718,000 | TZS 382,454,367 | 75 | Jumla ya 13,500m zimeshalazwa, |
| 3 | Ujenzi wa miundombinu ya maji eneo la Pangani (Mradi wa Miji 28) | USD 81,142,931 | USD 25,673,769 | 60 | Mradi utahudumia miji ya Korogwe, Handeni, Muheza na Pangani<br>Ujenzi wa Matanki matatu ya maji Pangani unaendelea (Madanga- 200c.m, Boza – 500c.m na Ubangaa-200c.m).<br>Ulazaji wa bomba la maji unaendelea hadi sasa jumla ya 9km zimelazwa kutoka Madanga hadi Boza |
| 4 | Uendelezaji wa Mtandao na ukarabati wa miundombinu ya maji (Hati Fungani – maeneo yote ya Tanga, Pangani na Muheza) | TZS 53,120,000,000 | | 8 | Pangani kutafanyika; Kuendeleza mabomba (15km)<br>Ukarabati wa mabomba (5km)<br>Maunganisho ya wateja (100) |
| 5. | Ujenzi wa mabwawa ya kupokea na kutibu majitaka na kutumia topetaka katika mjiwa Pangani. | TZS 995,519,897.54 | TZS 891,614,492.48 | 95 | Ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka umekamilika,<br>Ujenzi wa vyoo vya matundu 8 kila kimoja katika Shule ya msingi Funguni, Shule ya Sekondari Funguni na Kituo cha Mabasi Mjini - Pangani<br>Ununuzi wa gari moja la kunyonya majitaka<br>Ununuzi wa gari la usimamizi wa mradi |

## 14.1 WAKALA WA USAMBAZAJI MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI (RUWASA)

### 14.1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, RUWASA katika Wilaya ya Pangani inatekeleza majukumu yake kwa ushirikiano na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga UWASA Pamoja na Taasisi na Idara mbalimbali zilizopo katika Wilaya ya Pangani.

### 14.1.2 Rasilimali watu

**Watumishi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, RUWASA Wilaya ya Pangani kwa sasa ina jumla ya watumishi waajiriwa 12, Ambapo ina Wahandisi watatu (3), Fundi Sanifu mmoja (1), Fundi Sanifu Wasaidizi (5), Afisa Maendeleo ya Jamii (1), Msaidizi wa Ofisi (1) na Mwandishi Mwendesha Ofisi (1). Hata hivyo Ofisi ina watumishi 4 wa ajira ya mkataba na watumishi 4 ni wa *intership.*

### 14.1.3 Hali ya huduma ya maji (*Service Delivery*)

**Maeneo ya Vijijini**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka, 2022 Wilaya ya Pangani inakadiliwa kuwa na wakazi wapatao 75,642 ambapo kati ya hao RUWASA Wilaya ya Pangani ina hudumia wakazi wapatao 60,878 waliopo katika vijiji 29 kati ya Vijiji 33 vilivyopo Wilaya ya Pangani, ambapo Kata 4 zenye Vijiji 4 vyenye wakazi 14,764 vina hudumiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga - UWASA.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Wastani wa watu wanaopata huduma ya maji safi na salama hadi kufikia Disemba, 2024 ni watu 52,685 waishio katika Vijiji 27 sawa na asilimia 86.5 kati ya watu 60,878 waishio katika Vijiji 29 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ambapo Vijiji hivyo vinahudumiwa na RUWASA pia watu wanapata huduma ya maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Hata hivyo utekelezaji wa miradi ya maji **MKwaja, Kipumbwi, Tungamaa, Mrozo, Meka – Mseko, Sange na Mwembeni** inayoendelea kutekelezwa itakapo kamilika itapelekea upatikanaji wa huduma ya maji maeneo ya vijijini kufikia asilimia **95** sawa na wakazi 57,834 waishio vijijini. Vile vele Mradi Mkubwa wa Maji wa Miji 28 ambao unaendelea na utekelezaji utakapo kamilika utaondoa tatizo la maji katika Wilaya ya Pangani.

### 14.1.4 Utekelezaji wa miradi

**Miradi iliyotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika Mwaka wa Fedha **2023/2024** RUWASA Wilaya ya Pangani ilitengewa Bajeti ya Jumla ya **Shilingi 2,119,127,554.97** ambapo fedha zote zilipokelewa na kutumika katika utekelezaji wa miradi **13**, miradi miwili (2) ya **Mkalamo** na **Sakura/Kwakibuyu** ilikamilika wakati miradi 11 inaendelea nautekelezaji katika mwaka wa fedha 2024/2025 kama inavyoonekana katika taarifa zilizoambatanishwa ***Jedwali Na.1.***

**Miradi inayotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025**
**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika Mwaka wa Fedha **2024/2025** RUWASA Wilaya ya Pangani imetengewa Bajeti ya **Shilingi 3,312,974,072.26** ambapo kiasi cha **Shilingi704,914,719.26** ni Fedha kutoka **Mfuko wa Maji wa Taifa (NWF)** na kiasi cha **Shilingi 2,608,059,353** ni Fedha kutoka katika ***Program*** ya **PforR,** Ambapo Bajeti hii niongezeko la **Shilingi 1,193,846,517.29** ya bajeti ya mwaka **2023/2024.** Jumla ya miradi 13 itatekelezwa ambapo miradi 11 inaendelea na miradi 2 ni mipya kama inavyoonekana katika taarifa zilizoambatanishwa ***Jedwali Na. 2.***

### 14.1.5 Mradi wa Uchimbaji Visima vitano (5) kila Jimbo
**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Katika utatuzi wa haraka wa changamoto ya maji katika maeneo yasiyokuwa na huduma ya maji, Sekta ya maji inatekeleza Mpango wa uchimbaji visima 900 nchini ambapo kila Jimbo litachimbiwa visima 5 na kujenga *Point Source* ilihuduma ya maji ipatikane kwa haraka.
Katika Jimbo la Pangani maeneo 5 ya Vijiji vya Buyuni, Mivumoni, Langoni, Kovukovu na Mkalamo tayari yamechimbiwa visima ambapo Kijiji cha Buyuni yamepatikana maji yenye chumvi sana, Kovukovu maji yamekosekana, Langoni maji yamekosekana, Mivumoni maji ni machache sana na Mkalamo maji yamepatikana ya kutosha na salama kwa matumizi ya binadamu.

### 14.1.6 Usimamizi wa utoaji huduma ya maji
**Mheshimiwa Mwenyekiti**, jumla ya vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) 5, ambazo zimesajiliwa kwa kutumia sheria mpya Na.5 ya Mwaka 2019, na zinaendesha na kusimamia miradi ya maji Vijijini. CBWSO hizo ni MIKI MPYA, KIBUMA, TUMBWE, KIKWA na MKWA. Jedwali Na. 3 hapa chini linaelezea asilimia ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kila CBWSO.

**Jedwali Na.3**

| Na. | JINA LA CBWSO | ASILIMIA YA UPATIKANAJI MAJI | UPUNGUFU WA UPATIKANAJI MAJI |
|---|---|---|---|
| 1. | TUMBWE | 88% | 12% |
| 2. | KIBUMA | 87% | 13% |
| 3. | MIKI MPYA | 89.5% | 10.5% |
| 4. | MKWA | 78% | 22% |
| 5. | KIKWA | 90% | 10% |
| | **WASTANI** | **86.5%** | **13.5%** |

### 14.1.7 Malengo ya RUWASA Wilaya ya Pangani
**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Lengo kuu la Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) katika Wilaya ya Pangani ni kufikisha maji katika vijiji vyote ifikapo Desemba, 2025. Ambapo kwa sasa vijiji viwili (2) vya Buyuni na Mivumoni ndio havina miundombinu ya maji toshelevu japokuwa huduma ya maji ipo.

***Jedwali Na. 1*: Miradi iliyotekelezwa katika Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

| Na | Jina la Mradi | Mtekelezaji | Gharama ya Mradi | Fedha zilizopokelewa | Asilimia ya utekelezaji | Changamoto | Maelezo/Status |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa mradi wa maji Kwakibuyu - Sakura. | MATRIX TECHNOLOGY CO.LTD | 594,282,818.00 | 324,680,572.97 | 100 | Hakuna changamoto | Mradi umekamilika |
| 2 | Ujenzi wa mradi wa maji Mkalamo. | YAJUKI INVESTMENT CO. LTD | 507,402,957.00 | 426,300,869.40 | 100 | Hakuna changamoto | Mradi umekamilika |
| 3 | Ujenzi wa mradi wa maji Kipumbwi. | MATRIX TECHNOLOGY CO.LTD | 703,021,847.00 | 152,543,000.00 | 75 | Hakuna changamoto | Mkandarasi anaendelea na ukamilisahaji wa kazi katika Tanki, nyumba ya kufungia mitambo, CBWSO Ofisi na kukamilisha kulaza bomba. |
| 4 | Ujenzi wa mradi wa maji Mrozo. | KGG INVESTMENT LTD | 825,587,254.00 | 502,262,960.55 | 85 | Kwa sasa hakuna changamoto | Mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa kazi |
| 5 | Upanuzi na Ukarabati mradi wa maji Tungamaa. | Local Fund | 513,108,151.56 | 300,000,000.00 | 85 | Hakuna changamoto | Utekelezaji upo hatua ya ukamilishaji |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Ukarabati na Upanuzi wa mradi wa maji Sange. | Local Fund | 540,469,999.30 | 300,000,000.00 | 85 | Hakuna changamto | Utekelezaji upo hatua ya ukamilishaji |
| 7 | Ujenzi wa mradi wa maji Mwembeni. | Local Fund | 559,238,672.69 | 350,000,000.00 | 90 | | Inahitajika Tsh.50,000,000.00/= ya ukamilishaji kazi |
| 8 | Ujenzi wa mradi wa Maji Meka - Mseko. | Local Fund | 698,325,844.92 | 400,000,000.00 | 80 | Utekelezaji kazi unaendelea | Mradi umeanza kutoa huduma kwa wananchi |
| 10 | Mpango wa haraka wa uchimbaji visima 5 kwa kila Jimbo katika vijiji visivyo na maji. | RUWASA Kitengo cha Uchimbaji Visima | 300,000,000.00 | 300,000,000.00 | 40 | Umefanyika utafiti wa maji chini ya aridhi maeneo ya Kovukovu, Mivumoni, Buyuni, Mkalamo na Langoni | Visima 5 vitachimbwa na kuwekewa miundombinu ya kutoa maji ili huduma ipatikane hapo hapo, kabla ya kuya sambaza katika Kijiji kizima |
| 11 | Ukarabati mradi wa maji Bweni. | Locala Fundi | 317,850,165.59 | 215,000,000.00 | 70 | Hakuna changamoto | Kazi ya ukarabati mradi inaendelea |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12 | Ukarabati mradi wa maji Mzambarauni. | Locala Fundi | 173,907,577.99 | 115,000,000.00 | 70 | Hakuna changamoto | Kazi ya ukarabati mradi inaendelea |
| 13 | Ukarabati mradi wa maji Mwera. | Locala Fundi | 301,599,729.86 | 301,599,729.86 | 72 | Hakuna changamoto | Kazi ya ukarabati mradi inaendelea |
| | JUMLA | | 6,034,795,017.91 | 3,287,387,132.78 | | | |

***Jedwali Na. 2*: Miradi inayotekelezwa katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA BAJETI YA MWAKA 2024/2025 KUANZIA JULAI HADI DESEMBA, 2024 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **JINA LA MRADI /NAMBA YA MKATABA** | **MKANDARASI/FORCE ACCOUNT** | **GHARAMA YA MKATABA** | **FEDHA ZILIZOTUMIKA/POKELEWA** | **CHANZO CHA FEDHA** | **ASILIMIA YA UTEKELEZAJI (%)** | **Sababu za Kutokamilika** |
| 1 | Ujenzi wa mradi wa maji Mrozo AE-102/2021 - 22/TAG/W/44 | KGG INVESTMENT LTD, P.O BOX 24111 DAR ES SALAAM | 825,587,254.50 | 502,262,960.55 | NWF | 75 | Mkandarasi anadai malipo ya IPC Na.3 ya Tsh.131,212,474.63/= |
| 2 | Ujenzi wa mradi wa maji Kipumbwi AE-102/2021 - 22/TAG/W/42 | MATRIX TECHNOLOGY COMPANY LTD, P.O BOX 30302 DAR ES SALAAM | 703,021,847.83 | 317,774,971.29 | NWF | 80 | Mkandarasi amelipwa malipo ya IPC Na. 2 Tsh 163,358,256.5/=, na kazi zinaendelea kutekelezwa |
| 3 | Ujenzi wa mradi wa maji Mkwaja AE-102/2021 - 22/TAG/W/47 | M/S KHARTON TRADERS LIMITED,P.O BOX 14025, DAR ES SALAAM | 836,220,420.00 | 531,461,920.00 | NWF | 90 | Mkandarasi amelipwa Tsh.200,000,000.00/= na mradi unatoa huduma |
| 4 | Ujenzi wa mradi wa maji Meka - Mseko | FORCE ACCOUNT | 698,325,844.92 | 450,000,000.00 | NWF | 88 | Inahitajika kiasi cha Shilingi100,000,000.00/= kukamilisha kazi |
| 5 | Ujenzi wa mradi wa maji Mwembeni | FORCE ACCOUNT | 559,238,672.68 | 450,000,000.00 | NWF | 90 | Inahitajika kiasi cha Shilingi50,000,000.00/= kukamilisha kazi |
| 6 | Ukarabati na Upanuzi mradi wa maji Tungamaa | FORCE ACCOUNT | 513,108,151.56 | 450,000,000.00 | NWF | 95 | Upo hatua ya ukamilishaji na unafanya kazi |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Ukarabati na Upanuzi mradi wa maji Sange | FORCE ACCOUNT | 540,469,999.30 | 369,691,034.75 | NWF | 95 | Inahitajika Tsh.150, 000,000.00/= ilikuweza kukamilisha kazi, ikiwa ni pamoja na kuwalipa wazabuni |
| 8 | Ukarabati mradi wa maji Bweni | FORCE ACCOUNT | 317,850,165.59 | 205,810,000.00 | PforR | 90 | Vifaa vya ukamilishaji kazi vipo katika hatua ya manunuzi |
| 9 | Ukarabati mradi wa maji Mzambarauni | FORCE ACCOUNT | 173,907,577.99 | 115,447,000.00 | PforR | 90 | Vifaa vya ukamilishaji kazi vipo katika hatiua ya manunuzi. |
| 10 | Ukarabati mradi wa maji Mwera | FORCE ACCOUNT | 301,599,729.86 | 300,000,000.00 | PforR | 90 | Vifaa vya ukamilishaji kazi vipo Ktika hatua ya manunuzi |
| 11 | Ujenzi wa mradi wa maji Buyuni | FORCE ACCOUNT | 250,000,000.00 | 0.00 | PforR | 0 | Mradi haujaanza kutekelezwa kutokana na changamoto ya kukosa chanzo cha maji (kisima kirefu) kwani kisima kilichochimbwa kina maji ya chumvi |
| 12 | Ujenzi wa mradi wa maji Mivumoni | FORCE ACCOUNT | 376,447,482.40 | 0.00 | PforR | 0 | Mradi haujaanza kutekelezwa kutokana na changamoto ya kukosa chanzo cha maji (kisima kirefu) kwani kisima kilichochimbwa kina maji ya chumvi kwani kisima kilichochimbwa kina maji machache |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 13 | Mpango wa uchimbaji visima virefu 5 kila Jimbo na kuvijengea *Point source* | FORCE ACCOUNT | 300,000,000.00 | 175,000,000.00 | PforR | 50 | Hadi sasa vimechimbwa visima virefu 5, Kisima cha Mkalamo kina maji yakutosha, Mivumoni maji machache hayatoshi, Kovukovu na Langoni hakuna maji, Buyuni maji ni ya chumvi sana |
| | **JUMLA** | | **6,395,777,146.63** | **3,867,447,886.59** | | | |

## 15.0 SEKTA YA NISHATI (TANESCO)

### 15.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Pangani ni miongoni mwa Wilaya nane za mkoa wa Tanga. Inapata umeme kutoka Gridi ya Taifa (Msongo 132kv) kupitia vituo vya Kange (Tanga) na Songa (Korogwe) kupitia Muheza. Tuna kituo kidogo cha kupooza na kusambaza umeme cha Bushiri (33kv-11kv).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wilaya ya Pangani ina vijiji 33 na vyote tayari vimepatiwa umeme aidha, kati ya vitongoji 96 vilivyopo ndani ya Wilaya vitongoji 64 vimefikishiwa Huduma ya umeme. Vitongoji 32 vilivyosalia tayari mapendekezo ya kuomba kuwekwa kwenye mpango wa kupatiwa umeme yamekwisha wasilishwa REA.

#### 15.1.1 Mradi wa maeneo ya migodi, uwekezaji na umwagiliaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 Wilaya ya Pangani imekuwa miongoni mwa Wilaya 7 (Handeni, Lushoto, Korogwe, Mkinga, Muheza, Kilindi na Pangani) za Mkoa wa Tanga zilizofanikiwa kupata mradi wa usambazaji umeme maeneo ya migodi, viwanda na umwagiliaji. Mradi huo umenufaisha pia baadhi ya vitongoji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Jina la mradi huo ni **"Electrification of Small-Scale Mining, Industrial and Agricultural Areas in Mainland Tanzania"** chini ya ufadhili wa **Serikali ya Tanzania**. Mradi unasimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini **(REA)** ukiwa na thamani ya Shilingi za Kitanzania **Bilioni 2.1** kwa Wilaya ya Pangani. Mradi unatekelezwa na Mkandarasi mzawa **DIEYNEM COMPANY LTD** na kazi imekamilika kwa asilimia (100%) tangu mwezi Oktoba, 2024.

| Sno. | Eneo | Wigo 33Kv (km) | Wigo Laini ndogo | Transformer | Utekelezaji asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kipumbwi (Osterbay) | 0 | 1.5 | 1 | 100% |
| 2. | Pangani Magharibi | 0.28 | 1.4 | 1 | 100% |
| 3. | Mzinga Plantation | 9.2 | 0 | 1 | 100% |
| 4. | Boza | 0.4 | 1.7 | 1 | 100% |
| 5. | Serewani | 0.8 | 0.6 | 1 | 100% |
| 6. | Aweso Secondari/Jasini | 1.7 | 1 | 1 | 100% |
| 7. | Chamwino Mkaramo | 0 | 0.5 | 1 | 100% |
| 8. | Mnazi mmoja | 1.6 | 1.5 | 1 | 100% |
| 9. | Kikokwe | 5.4 | 0 | 0 | 100% |
| 10. | Choba | 3.3 | 0 | 0 | 100% |
| 11. | Mwembeni | 0.5 | 1.3 | 1 | 100% |
| 12. | Mwembe Kodi | 0.8 | 0 | 0 | 100% |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mpaka sasa wateja/kaya zaidi ya 142 zimenufaika na mradi ikiwemo maeneo mawili ya uwekezaji pamoja na shule ya Sekondari 1.

### 15.1.2 Utekelezaji wa miradi bajeti za ndani

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Bajeti ya mwaka 2024 – 2025 tumepeleka umeme katika maeneo mawili kwa mchanganuo katika jedwali,

| Na. | Maelezo | Thamani (Tsh) | Wanufaika |
|---|---|---|---|
| 1. | Usambazaji umeme na uwekaji wa Transformer eneo la Choba | 28,049,233.07 | Wananchi/kaya zaidi ya 70 wamenufaika. |
| 2. | Upelekaji umeme eneo la uwekezaji Kibinda (Amboni Sisal Properties LTD) | 59,055,859.22 | Muwekezaji pamoja na wanachi |

### 15.1.3 Faida za miradi

1. Kuunganisha miradi ya uwekezaji na umeme ili kukuza uchumi pamoja na kuongeza ajira kwa lengo la kukuza kipato cha wananchi katika maeneo hayo.
2. Kusogeza huduma kwa wananchi na kusaidia kuendesha biashara kisasa.
3. Kuboresha masuala ya kiuongozi na uzalishaji kwenye viwanda vidogo, biashara ndogondogo na migodi midogo ikiwemo maeneo ya miradi.
4. Kupunguza hali ya umasikini maeneo ya miradi

## 16.0 SEKTA YA BARABARA

### 16.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Pangani ina mtandao wa barabara wa jumla ya kilometer 408.64 kati ya hizo kilometa 63 ni za Mjazio (Feeeder Roads), kilometa 204.71 ni za mkusanyo (Colletor Roads) na kilometa 79.32 ni za jamii/kijiji (Community Road).

### 16.2 Hali ya barabara

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hali ya barabara zetu ni ya wastani na maeneo mengi hupitika hata wakati wa mvua kama ilivyoainishwa hapa chini;

Asilimia 37.59 ni nzuri (kilometa 153.6)

Asilimia 52.32 ni za wastanii (kilometa 214.83)

Asilimia 10.09 ni mbaya hupitika kwa shida (kilometa 40.21)

Pia tabaka la juu la barabara hizi ni kama ifuatavyo;

Asilimia 1.46 ni za lami (kilometa 5.98)

Asilimia 58.91 ni za moramu (kilometa 240.75)

Asilimia 39.63 ni za udongo (kilometa 161.91)

### 16.3 Mpango wa utekelezaji uliovuka mwaka 2023/2024 ulioidhinishwa

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Mwaka wa fedha **2023/2024** TARURA(W) Pangania ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,774,530,000** kwa ajili ya matengenezo ya jumla ya **km 170.87, makalvati na madaraja 10 na mitaro 400m** lakini hadi Juni 30, Mwaka 2024 miradi iliyovuka Mwaka ni ya thamani ya **Shilingi 2,568,309,969** kutoka kwenye vyanzo vinne **(4)** kama ifuatavyo;

#### 16.3.1 Fedha za Matengenezo kutoka Mfuko wa Barabara (Maintenance)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bajeti iliyoidhinishwa ni **Shilingi 1,024,530,000** ikihusisha matengenezo ya barabara km 117.81 na Usimamizi lakini miradi iliyovuka Mwaka 2023/2024 ni ya thamani ya **Shilingi 564,271,901.**

#### 16.3.2 Fedha za Maendeleo za Mfuko wa Jimbo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bajeti iliyoidhinishwa ni **Shilingi 500,000,000** ikihusisha matengenezo ya barabara km 0.9 kwa kiwango cha lami na Usimamizi lakini miradi iliyovuka Mwaka 2023/2024 ni ya thamani ya **Shilingi 474,010,400**

#### 16.3.3 Fedha za Maendeleo za Zitokanazo na Tozo ya mafuta

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bajeti iliyoidhinishwa ni Shilingi 1,250,000,000 ikihusisha matengenezo ya barabara km 52.16 na Usimamizi lakini miradi iliyovuka Mwaka 2023/2024 ni ya thamani ya **Shilingi 1,177,888,504.**

#### 16.3.4 Vyanzo vingine vya fedha vilivyovuka Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Mwaka wa fedha **2023/2024** TARURA(W) Pangani iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 360,739,560,** hata hivyo miradi iliyovuka Mwaka 2023/2024 ina thamani ya **Shilingi 352,139,164** kutokana na vyanzo vingine kama ifuatavyo;

- Fedha za dharura (mfuko wa barabara) km 0.5 na kavati 7 Shilingi 129,975,000
- Fedha za wafadhili (World Bank/RISE) km 7 Shilingi 222,164,164
- **JUMLA** **Shilingi 352,139,164**

### 16.4 Mapokezi ya fedha kwa mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika kipindi cha Julai – Desemba 2024 jumla ya fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 329,950,340** ama fedha zote za Mwaka 2023/2024 kufikia **Shilingi 1,077,082,305** sawa na asilimia **39%** kati ya **shilingi 2,774,530,000** na **f**edha ambazo bado hazijaletwa ni **shilingi 1,697,447,695** ni sawa na asilimia 61% mchanganuo wa mapokezi ni kama ifuatavyo;

- Fedha za Matengenezo (maintenance) Shilingi 393,577,694.00
- Fedha za maendeleo za Jimbo Shilingi 156,769,021.00
- Fedha za Tozo ya mafuta Shilingi 479,196,450.00
- Fedha za Dharura Shilingi 47,539,140.70
- **JUMLA** **Shilingi 1,077,082,305**

### 16.5 Utekelezaji wa kazi za mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Utekelezaji wa kazi umeainishwa kutokana na vyanzo vya fedha kama ifuatavyo;

#### 16.5.1 Kazi za matengenezo (Maintenance)

Kazi za matengenezo ambazo miradi iliyovuka Juni 30, mwaka 2024 ni ya thamani ya **Shilingi 564,271,901** utekelezaji wake umefikia wastani wa **84%** ya utekelezaji. ***Kiambatanisho Na.1 kinaonyesha, uk. 53***

#### 16.5.2 Miradi ya Maendeleo kwa kila Jimbo

Kazi za miradi ya maendeleo kutoka serikali kuu kwa kila jimbo ambazo miradi iliyovuka Juni 30, mwaka 2024 ni ya thamani ya **Shilingi 474,010,400** utekelezaji wake umefikia wastani wa **70%** ya utekelezaji. ***Kiambatanisho Na.2 kinaonyesha, uk. 54***

#### 16.5.3 Miradi ya Maendeleo ya fedha zitokanazo na Tozo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kazi za miradi ya maendeleo kutoka serikali kuu fedha zitokanazo na Tozo ya mafuta ambazo miradi iliyovuka Juni 30, mwaka 2024 ni ya thamani ya Shilingi **1,177,888,504** utekelezaji wake umefikia wastani wa **63%** ya utekelezaji. ***Kiambatanisho Na.3 kinaonyesha, uk 54,55***

#### 16.5.4 Miradi ya Dharura (Mfuko wa barabara)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kazi za miradi dharura ya mfuko wa barabara ambazo miradi iliyovuka Juni 30, mwaka 2024 ni ya thamani ya **Shilingi 129,975,000** utekelezaji wake umefikia wastani wa **75%** ya utekelezaji. ***Kiambatanisho Na.4 kinaonyesha, uk 56***

#### 16.5.5 Miradi ya Wafadhili (World Bank)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kazi za miradi dharura ya mfuko wa barabara ambazo miradi iliyovuka Juni 30, mwaka 2024 ni ya thamani ya **Shilingi 222,164,164** utekelezaji wake umefikia wastani wa **32%.** *Kiambatanisho* ***Na.5 kinaonyesha, uk 56***

### 16.6 Utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya barabara ulioidhinishwa kwa mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika Mwaka wa fedha **2024/2025** TARURA (W) Pangani imeidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,774,530,000** kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye jumla ya **km 92.47, makalvati na madaraja 156 na mitaro 1340m** kutoka kwenye vyanzo vitatu **(3)** ambapo utekelezaji ni kuwa kazi zenye ukubwa wa asilimia 76% sawa na **Shilingi 1,897,056,000** ya mpango mzima zimetangazwa na kuingiwa mikataba na utekelezaji wake upo hatua mbalimbali kama ifuatavyo;

### 16.6.1 Kazi za matengenezo (Maintenance)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kazi za matengenezo ambazo bajeti yake ni **Shilingi 1,024,530,000** zimeingiwa mikataba kwa **asilimia 60** sawa na **Shilingi 538,233,000** na utekelezaji wake unaendelea kwa wastani wa utekelezaji wa 47% ***Kiambatanisho Na.6 kinaonyesha, uk.57,58***

### 16.6.2 Miradi ya Maendeleo kwa kila Jimbo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kazi za miradi ya maendeleo kutoka serikali kuu kwa kila jimbo ambazo bajeti yake ni **Shilingi 500,000,000** zimeingiwa mikataba kwa asilimia **100** sawa na **Shilingi 474,894,000** na utekelezaji wake unaendelea sawa na 25%. ***KiambatanishoNa.7 kinaonyesha, uk. 59***

### 16.6.3 Miradi ya Maendeleo ya fedha zitokanazo na Tozo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kazi za miradi ya maendeleo kutoka serikali kuu fedha zitokanazo na Tozo ya mafuta ambazo bajeti ni **Shilingi 1,250,000,000** zimeingiwa mikataba kwa **asilimia 80** sawa na **Shilingi 883,929,000** na utekelezaji wake unaendelea kwa wastani wa 25%. ***Kiambatanisho Na.8 kinaonyesha, uk. 59,60***

### 16.7 Mapokezi ya fedha kwa mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Katika kipindi cha Julai - Disemba 2024 zimepokelewa jumla ya kiasi cha **Shilingi 195,959,376 kwa ajili ya Utawala** na malipo ya awali ya Wakandarasi kwa Mwaka 2024/2025 sawa na asilimia **7.1%** kati ya shilingi **2,774,530,000** zilizopangwa.

*KIAMBATISHO NA.1: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MATENGENEZO (MAINTENANCE) YA BARABARA- MFUKO WA BARABARA KWA MPANGO ULIOVUKA MWAKA 2023/2024*

| Na. | Jina la Mradi na namba ya Mkataba | Jina La Kampuni | Gharama ya Mkataba | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Fedha Zlizolipwa | Hali ya Mradi kwa sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matengenezo ya kawaida na sehemu korofi barabara za Langoni - Kirupu, Kasanga - Mtonga na Stahabu - Stahabu – Pwani, S10/026/2023/2024/W/121 | M/S SUPER TECNO ENGINEERING LIMITED P.O BOX 31828 DSM | 166,471,900 | 11/09/2023 | 30/01/2025 | 0 | Utekelezaji wa kazi umefikia 68% |
| 2 | Matengenezo ya kawaida na sehemu korofi barabara za Sakura - Mtango No.2, Kipumbwi Pr/School, Makorora - Sange No.2, S10/026/2023/2024/W/126 | MWANAFUNYO COMPANY LIMITED, BOX 155 LUSHOTO | 93,011,000 | 11/09/2023 | 15/01/2025 | 81,624,880 | Utekelezaji wa kazi umefikia 96% |
| 3 | Upgrading of Sinani Road to Bitumen Standard - S10/026/2023/2024/W/99 | M/s Peace Construction Limited, P.O. Box 105013 DSM | 217,609,001 | 11/09/2023 | 27/01/2025 | 79,687,375 | Utekelezaji wa kazi umefikia 70% |
| 4 | Matengenezo kiwango cha Lami (Second seal na mitaro) Phase II, barabara ya Sinani, S10/026/2023/2024/W/181 | M/s Peace Construction Limited, P.O. Box 105013 DSM | 87,180,000 | 22/04/2024 | 24/01/2025 | 0 | Utekelezaji wa kazi umefikia 30% |
| | | | 564,271,901 | | | 161,312,255 | |

*KIAMBATISHO NA.2: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO (DEVELOPMENT) KWA FEDHA ZA MFUKO WA JIMBO KWA MPANGO ULIOVUKA MWAKA 2023/2024*

| Na. | Jina la Mradi na namba ya Mkataba | Jina La Kampuni | Gharama ya Mkataba | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Fedha Zlizolipwa | Hali ya Mradi kwa sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matengenezo kiwango cha lami barabara za Bakwata No.1 na Mnyongeni S10/026/2023/2024/W/108 | M/S PEACE CONSTRUCTION LIMITED P.O BOX 105013, DSM | 474,010,400 | 11/09/2023 | 10/01/2025 | 156,769,021 | Utekelezaji wa kazi umefikia 70% |

*KIAMBATISHO NA.3: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO (DEVELOPMENT) KWA FEDHA ZA TOZO*

*KWA MPANGO ULIOVUKA MWAKA 2023/2024*

| Na. | Jina la Mradi na namba ya Mkataba | Jina La Kampuni | Gharama ya Mkataba | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Fedha Zlizolipwa | Hali ya Mradi kwa sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa mitaro barabara za Bakwata No.1 na Ferry - Mnyongeni Phase II- S10/026/2023/2024/W/180 | M/S PEACE CONSTRUCTION LIMITED P.O BOX 105013, DSM | 187,469,500 | 15/04/2024 | 30/01/2025 | 68,587,110 | Utekelezaji wa kazi umefikia 63% |
| 2 | Matengenezo ya muda maalum barabara za Sakura – Kipumbwimtoni, Mwera – Ushongo na Mwera - Kirupu S10/026/2023/2024/W/120 | M/s IKOVOKOVO CONSTRUCTION LTD, P.O.BOX 75, MAKETE | 195,706,400 | 11/09/2023 | 30/01/2025 | 136,825,000 | Utekelezaji wa kazi umefikia 84% |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Matengenezo ya muda maalum barabara za Madanga - Mtiti, Bago -Madanga, Boza - Mnazi mmoja - Madanga, na Mivumoni - Mapojoni<br><br>S10/026/2023/2024/W/114 | DIGOTECH CIVIL WORKS COMPANY LIMITED, Box 8716 MOSHI | 263,923,203.7 | 17/01/2024 | 20/01/2025 | 39,588,480 | Utekelezaji wa kazi umefikia 32% |
| 4 | Matengenezo ya muda maalum barabara za Masaika - Kovukovu road, Kijiweni - Pombwe, Kigurusimba - Pombwe, Matakani - Kijiweni, na Choba No.6, S10/026/2023/2024/W/116 | VALOSU COMPANY LTD<br><br>Box 1588, MWANZA | 288,766,000 | 17/01/2024 | 20/01/2025 | 137,892,350 | Utekelezaji wa kazi umefikia 80% |
| 5 | Matengenezo ya muda maalum barabara ya Mwera-Gendagenda 14km, Contract No.<br><br>S10/026/2023/2024/W/117 | Suma JKT Construction Co. Ltd<br><br>Box 1694<br><br>DSM | 242,023,400 | 15/05/2024 | 11/02/2025 | 36,303,510 | Utekelezaji wa kazi umefikia 28% |
| | | | 1,177,888,504 | | | **419,196,450** | |

*KIAMBATISHO NA.4: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA DHARURA (MFUKO WA BARABARA) KWA MPANGO ULIOVUKA MWAKA 2023/2024*

| Na. | Jina la Mradi na namba ya Mkataba | Jina La Kampuni | Gharama ya Mkataba | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Fedha Zlizolipwa | Hali ya Mradi kwa sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kunyanyua tuta la Barabara na Makalvati katika Barabara za Istiqama na Mbulizaga – Mkalamo, S10/026/2023/2024/W/185 | M/s Peace Construction Limited, P.O. Box 105013 DSM | 129,975,000 | 6/05/2024 | 18/01/2025 | 47,539,140.70 | Utekelezaji wa kazi umefikia 75% |
| | **JUMLA** | | **129,975,000** | | | **47,539,140.70** | |

*KIAMBATISHO NA.5: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WAFADHILI (WORLD BANK) KWA MPANGO ULIOVUKA MWAKA 2023/2024*

| Na. | Jina la Mradi na namba ya Mkataba | Jina La Kampuni | Gharama ya Mkataba | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Fedha Zlizolipwa | Hali ya Mradi kwa sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matengenezo ya barabara ya Mwera – Gendagenda kiwango cha moramu 7km, contract. AE.092/WB-RISE/2022/23/W/01 | M/S Yota Enterprises Ltd | 222,164,164 | 15/05/2024 | 10/01/2025 | 0 | Utekelezaji wa kazi umefikia 32% |
| | **JUMLA** | | **222,164,164** | | | 0 | |

# MPANGO WA MATENGENEZO YA BARABARA ULIOIDHINISHWA KWA MWAKA 2024/2025 NA UTEKELEZAJI WAKE

***KIAMBATISHO NA.6: MIRADI YA MATENGENEZO (MAINTENANCE)- MFUKO WA BARABARA***

| Na | Jina la Mradi | Jina la Mkandarasi | Gharama ya Mkataba/ Bajeti (Shilingi) | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Fedha zilizolipwa (Shilingi) | Hatua ya utekelezaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matengenezo ya kawada, sehemu korofi, muda maalum na makalvati barabara za Mjipya - Mbulizaga 3.75km, Mkalamo - Mhungulu 1.8km, na Mbulizaga - Mkalamo 7.2km, Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/16 | Muka Techno Ltd, Box 70572 DSM | 186,132,500 | 19/8/2024 | 15/2/2025 | 0 | Utekelezaji umefikia 38% |
| 2 | Matengenezo ya kawada, sehemu korofi, muda maalum na makalvati barabara za Mkoba road 1.0km , Ngaa road 0.8km, Gombero road No.1, 0.7km, Bakwata road No.2, 0.44km , Funguni road No.1, 0.95km, Ngongo road 0.5km, Istiqama road No.2 , Mhembo road No.6, 0.26km, Mnyongeni road 0.4km, Boza – Muhembo road 0.8km, New Mnyongeni road 0.5km, Majengo mapya No.2 road, 0.44km, & Maziwe road, Mkataba Na. 0.2km S10/026/2024/2025/W/22 | Sasha Group, Box 1579, Tanga | 240,696,500 | 22/8/2024 | 18/2/2025 | 0 | Utekelezaji umefikia 40% |
| 3 | Ujenzi wa Mitaro 320m barabara ya Kibwengo na 120m barabara ya Pangadeco No.2, 240m barabara ya Jamhuri road (Labour Based | Sasha Group, Box 1579, Tanga | 55,790,000 | 15/8/2024 | 11/2/2025 | 0 | Utekelezaji umefikia 70% |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Technology), Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/24 | | | | | | |
| 4 | Ujenzi wa Mitaro 240m barabara ya Kisima mbigili, 100m Funguni.2, & 320m barabara ya Majimaji (Labour Based Technology), Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/28 | Sasha Group,<br>Box 1579, Tanga | 55,614,000 | 14/8/2024 | 10/2/2025 | 0 | Utekelezaji umefikia 75% |
| 5 | Matengenezo ya kawada, sehemu korofi, muda maalum na makalvati barabara za Mwera - Tungamaa 3.10km, Mahakamani 1.04km, Meka - Mafisi 2.5km, na Langoni - Forest - Mtango 6.3km, Zabuni Na. S10/026/2024/2025/W/19 | | 207,640,000 | | | 0 | Kazi ipo hatua ya maandalizi ya nyaraka za zabuni |
| 6 | Matengenezo ya kawada, sehemu korofi, muda maalum na makalvati barabara za Sahanini - Msaraza 3.26km, Masaika - Kovukovu 7.6km, Boza Road No.3, 1.36km, Mkoma Road No.3, 1.36km, Kimanga - Madanga 3.65km, na Ferry-Kumbamtoni Road, Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/21 | | 200,120,000 | | | 0 | Kazi ipo hatua ya maandalizi ya nyaraka za zabuni |
| | | | **921,513,000** (pamoja na miradi ambayo haijatangazwa)<br>**538,233,000** (Mikataba inayoendelea) | | | | **Utekelezaji umefikia 47%** |

*KIAMBATISHO NA.7: MIRADI YA MAENDELEO (SERIKALI KUU - JIMBO)*

| Na | Jina la Mradi | Jina la Mkandarasi | Gharama ya Mkataba (Shilingi)) | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Fedha zilizolipwa (Shilingi) | Hatua ya utekelezaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matengenezo ya barabara ya Mnyongeni kwa kiwango cha lami 0.84km, Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/26 | Atimo Contractor's Ltd, Box 5304, Tanga | 474,894,000 | 16/8/2024 | 12/2/2025 | 0 | Utekelezaji umefikia 25% |
| | JUMLA | | **474,894,000** | | | | |

*KIAMBATISHO NA.8: MIRADI YA MAENDELEO (DEVELOPMENT) FEDHA ZITOKANAZO NA TOZO*

| Na | Jina la Mradi | Jina la Mkandarasi | Gharama ya Mkataba | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya kumaliza | Fedha zilizolipwa (Shilingi) | Hatua ya utekelezaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi barabara za Masaika - Kigurusimba 15.7km, Mivumoni - Kigurusimba 6.6km, na Masaika - Mrozo 11.7km, Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/31 | Quantec Ltd, Box 457, Kahama | 591,849,000 | 14/8/2024 | 10/2/2025 | 88,777,350 | Kazi imefikia 30% inaendelea |
| 2 | Matengenezo ya muda maalum barabara za Bweni - Mseko 7km na Bweni – Mkwajuni 2.5km, Mkataba Na. S10/026/2024/2025/W/32 | Jeitech Contractor Ltd, Box 705572, DSM | 292,080,000 | 15/8/2024 | 11/2/2025 | 43,812,000 | Kazi imefikia 25% inaendelea |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Matengenezo ya muda maalum barabara ya Bweni - Kikomwe - Mwera 3.2km na Ujenzi wa boksi kalvati barabara ya Langoni – Kirupu na Mwera – Kirupu, Zabuni Na. S10/026/2024/2025/W/78 | | 229,000,000 | | | 0 | Kazi ipo hatua ya maandalizi ya nyaraka za zabuni |
| | **JUMLA** | | **1,112,929,000** (Pamoja na miradi ambayo haijatangazwa) **883,929,000** (Mikataba inayoendelea) | | | **132,589,350** | |

## 17.0 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) -PANGANI

### 17.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mamlaka ya Mapato Tanzania (kama inavyotamkwa "Mamlaka) ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kwa sheria Na.11 ya mwaka 1995 na kuipa jukumu la kuwa taasisi kuu ya kukadiria, kukusanya mapato na kusimamia utekelezaji wa sheria za kikodi za mapato husika. Mabadiliko ya sheria mbalimbali kutokana na bajeti za kila mwaka yameendelea kuiongezea majukumu Mamlaka ya Mapato katika ukusanyaji wa kodi, tozo, ushuru na ada mbalimbali mfano: Kodi ya zuio katika huduma za kiutawala, kiufundi (Uchimbaji madini, mafuta na gesi) kwa wakazi na malipo kwa ajili ya manunuzi ya madini ya metali za thamani (Sheria ya Fedha 2023)**.**

### 17.2 Aina za kodi zinazokusanywa katika Wilaya: -

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kutokana na vyanzo mbalimbali vilivyoainishwa katika jedwali hapo juu wilaya tunakusanya kodi zifuatazo: -

#### 17.2.1 Idara ya Kodi za Ndani

**Direct taxes:** -

- Kodi za wafanyabiashara binafsi (Personal Income Tax, & Presumptive Bands).
- Kodi za Mapato ya Makampuni (Corporate taxes).
- Kodi za Mapato ya ajira (Employment taxes, PAYE & SDL).
- Kodi za zuio kwenye malipo ya Huduma na Bidhaa (WHT on G&S).
- Kodi ya zuio kwenye mikataba ya upangishaji (WHT on Rental).
- Tozo ya Kitanda Siku (Bed Night Levy).

**Indirect Taxes: -**

- Kodi ya Ongezeko la Thamani, (VAT).
- Ushuru wa Stempu (Stamp Duty)

#### 17.2.2. Idara ya Forodha

- Kodi ya uchakavu (Excise duty)
- Kodi ya bidhaa (Import duty)
- Kodi ya ongezeko la dhamani (VAT)
- Ushuru wa mabolesho ya reli (Railway development levy)

### 17.3 Utendaji kwa jumla kwa kipindi cha julai,2024 hadi desemba,2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa kipindi cha Julai,2024 hadi Desemba,2024, wilaya kwa idara zote zilipangiwa kukusanya Kodi za ndani na Ushuru wa Forodha kiasi cha Shilingi **3,911,412,565.30** ikihusisha Idara ya Kodi za ndani Shilingi **1,211,412,565.30** na Idara ya Ushuru wa Forodha Shilingi **2,700,000,000.00** Makusanyo kwa idarazote mbili ni shilingi **4,617,207,084.85** sawa na asilimia 118% ya lengo. Kama inavyojionyesha katika jedwali namba 1.

**Jedwali 1: Lengo la makusanyo ya kodi kwa kipindi cha Julai, 2023 mpaka Mei, 2024**

| IDARA | LENGO |
|---|---:|
| KODI ZA NDANI | 1,211,412,565.30 |
| FORODHA | 2,700,000,000.00 |
| **JUMLA** | **3,911,412,565.30** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 mpaka Desemba, 2024 wilaya imefanikiwa kukusanya shiligi **4,617,207,084.85** kati ya lengo la shilingi **3,911,412,565.30** ambayo ni sawa asilimia **118%** ya utendaji, Mchanganuo wa makusanyo ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 2.

**Jedwali 2: Malengo na Makusanyo kutoka Julai,2023 mpaka Mei,2024**

| IDARA | LENGO | MAKUSANYO HALISI | KIWANGO CHA UTENDAJI |
|---|---:|---|:---:|
| KODI ZA NDANI | 1,211,412,565.30 | 1,262,802,843.85 | 104% |
| FORODHA | 2,700,000,000.00 | 3,354,404,241.00 | 124% |
| **JUMLA** | **3,911,412,565.30** | **4,617,207,084.85** | **118%** |

### 17.4 Utendaji kwa idara ya kodi za ndani

### 17.4.1 Idara ya Kodi za Ndani,

- Kuongeza vyanzo vipya na kuimarisha vilivyokuwepo ili kuongeza tija na ufanisi katika ukusanyaji wake mfano, Kodi ya zuio katika upangishaji wa sehemu za biashara, kodi ya zuio ya huduma na bidhaa.
- Kuendelea kuhamasisha na kuboresha elimu kwa mlipakodi ambayo inachochea ulipaji kodi wa hiari, mfano matumizi ya mfumo wa E-filing, Online TIN registrations n.k.

- Ongezeko la usimamizi na ukaguzi wa wafanyabiashara wanaoandaa mahesabu ya mizania na wale ambao walipaswa kuanda hizo hesabu za mizania.
- Kuongeza usimamizi kwa wafanyabiashara wanaotumia mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) ambapo ni kwakutoa onyo na adhabu kwa wasiotoa risiti za kielektroniki (EFD) kwani ni njia nzuri yakupata mauzo ghaafi halali ya mlipa kodi kwa ajili ya makadilio ya

### 17.4.2 Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa

- Inaendelea na kufanya doria katika ukanda wa bahari kuhakikisha bidhaa zinaingizwa nchini kwa njia rasmi ili kuweza kulinda afya za watumiaji pamoja na kulinda viwanda vya ndani.
- Inaendelea na kuwezesha wafanyabiashara kupitisha bidhaa mbalimbali kwaajili ya masoko ya nje.
- Kukusanya mapato/kodi/ushuru kwa mizigo iliopitishwa kwa njia sahihi za kiforodha kwani ni lengo kuu la Mamlaka

### 17.5 Mikakati ya kufikia malengo ya mwaka, 2024/2025

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mikakati imejikita kuweka mipango kazi ya kila mwezi/wiki na siku ambao itatuwezesha kufika na kuvuka lengo. Mikakati tuliyojiwekea ni pamoja na: -

- Kufuatilia kwa karibu utumiaji wa mashine za EFD kwa lengo la kupanua vyanzo vipya vya kodi, mfano VAT, na uandaaji wa hesabu.
- Kuimarisha ushirikiano na taasisi nyingine za serikali katika kutambua vyanzo vya kodi, wakwepa kodi na utoaji wa elimu juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi yetu.
- Kusimamia ukadiriaji wa kodi ili kuhakikisha wafanyabiashara wote wanakadiriwa na kulipa kodi kwa wakati.
- Kufuatilia kwa karibu makato na ulipaji wa kodi za zuio kutokana na ushuru wa huduma/bidhaa kwa taasisi za serikali (shule na H/mashari, Vituo vya afya), Kampuni na biashara binafsi.
- Utambuzi, usajili, uelimishaji na ufuatiliaji wa sekta isiyo rasmi, mfano vikundi vya wajasiriamali, kuwezesha kuchangia mapato ya serikali.
- Kusimamia ubunifu, kujituma, uadilifu na uaminifu katika utendaji wetu wa kila siku.
- Kusimamia utoaji huduma bora kwa wateja, wadau na jamii nzima ili kuongeza ari na ridhaa ya utekelezaji wa sheria za kodi.

- Kufanya ukaguzi wa VAT, (VAT Control Verification exercise), kwa wafanyabiashara waliosajiliwa katika mfumo wa VAT.
- Kuandaa semina za mara kwa mara kwa ajili ya kutoa elimu kwa mlipa kodi kwa lengo kuelimisha, kutambua wajibu na haki zao, kusikiliza, kupokea na kutatua changamoto zao ili kuongeza ufanisi wa biashara na kuboresha ukusanyaji wa kodi.
- Kuanisha wafanya biashara wapya walio kidhi vigezo (threshold) ya kununua mashine za EFD na kuwasimamia wanunue na kuzitumia kwa ufasaha.
- Kuanisha wafanya biashara walio fikia kiwango (threshold) ya kusajiriwa VAT na kuwasajiri.

### 17.6 Changamoto zinazokabili Wilaya

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi kilichopita, Wilaya inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

| Na | Changamoto | Mapendekezo | Matarajio |
|---|---|---|---|
| 1. | Kukosekana kwa utamaduni wa utunzaji wa kumbukumbu na taarifa sahihi za biashara kwa wafanyabiashara. | Elimu kwa mlipakodi inaendelea kutolewa.<br><br>Viongozi wa serikali, Mh. DC, DAS, DED kutoa hamasa na kuwa sehemu ya kuhamasisha jamii juu ya utunzaji kumbukumbu za | Uboreshaji wa ukadiriaji wa mapato ya kodi<br><br>Kuboresha makusanyo ya kodi na yasiyo ya kikodi. |
| 2. | Hamasa ya chini kwa wananchi wengi kudai risiti wanaponunua bidhaa au kupata huduma sehemu mbalimbali. | Pamoja na jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Mapato, tunaomba viongozi wanapopata wasaa wa kuzungumza na wananchi kutoa hamasa ili kuongeza mwamko wa wananchi katika kudai risiti pindi wanapofanya manunuzi mbalimbali. | Upatikanaji wa taarifa sahihi za mauzo kwa wafanyabiashara zitakazosaidia ukadiriaji na ulipaji sahihi wa kodi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Udanganyifu wa utumiaji wa mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) hasa kwa walipa kodi waliosajiliwa katika kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambapo wakishasajiliwa wanashusha mauzo iliwaweze tolea katika kodi hiyo au pale wanapotakiwa kusajiliwa kutoa risiti chache ili kiwango kisifikiwe. | Pamoja na ukaguzi wa hesabu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato kubaini udanganyifu, tunaomba viongozi wanapopata wasaa wa kuzungumza na wananchi kutoa hamasa ili kuongeza mwamko wa walipa kodi kufuata sheria husika katika biashara zao hasa utoaji halali wa risiti za kielektroniki (EFD). | Utoaji wa elimu na adhabu kwa watakao fanya udanganyifu huo kwani wanapotosha Mamlaka kwa kutumia taarifa zisizo sahihi katika kupanua vyanzo vipya vya kodi. |
| 4. | Kodi kutolipwa kwa wakati ambazo ni kodi za awamu na madeni yanayatokana na ukaguzi wa hesabu za mizania. | Kufuatilia madeni hayo kwa kufuata taratibu za kisheria na utoaji wa adhabu ya usheleweshaji wa kodi kwa wakati. | Kutumia hatua kali za kisheria za ufuatiliaji ikiwemo kusimamisha matumizi ya akaunti za benki na kutaifisha mali ilikuweza kukomboa madeni hayo. |

## 18.0 MAMLAKA YA BANDARI

### 18.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bandari ya Tanga ni miongoni mwa Bandari kuu tatu (3) za mwambao wa bahari ya Hindi, zilizo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA); iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bandari No.17 ya mwaka 2004. Kupitia Sheria hiyo, kifungu cha 12 (1) (a) hadi (w) kinaipa nguvu za kisheria TPA kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo uendelezaji wa Bandari zote Tanzania zikiwemo zile zilizoko katika maziwa na mito.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Bandari ya Tanga inasimamia Bandari ndogo nne ambazo ni Pangani, Mkwaja, Kipumbwi zilzinazopatika Wilaya ya Pangani pamoja na Sahare iliyopo Wilaya ya Tanga. Pwani hii ya Bahari katika Mkoa wa Tanga ina umbali wa Kilomita za mraba zinazokadiriwa kuwa 700 na hivyo kupelekea uwepo wa Bandari bubu nyingi zisizo rasmi zinazofika takribani Bandari 50. Aidha, uwepo wa Bandari bubu imeleta changamoto ya usalama wa nchi, biashara ya magendo, uingizaji wa bidhaa zisizo ruhusiwa kwa njia za panya na kukosesha Serikali mapato.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari (TPA) ilianza kukusanya mapato katika Bandari hizi ndogo za Kipumbwi na Mkwaja kuanzia mwezi Novemba, 2019 baada ya kufanya tathmini

mbalimbali na kujiridhisha uwepo wa mizigo ya kutosha, na kuweka mkakati wa jinsi ya kukusanya mapato ambayo yalikuwa yanapotea kabla ya urasimishwaji wa Bandari hizo.

### 18.2 Hali ya utendaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hali ya utendaji katika kuhudumia shehena katika Bandari hizi ndogo za Pangani, Mkwaja na Kipumbwi kwa kipindi cha Oktoba – Disemba 2024 ni kama ifuatavyo:

**Jedwali No. 1 Shehena**

| Iliyopakiwa | Lengo Jul-Dis 2024 (Tons) | Halisi Jul-Dis 2024 (Tons) | Tofauti (Tons) | % |
|---|---|---|---|---|
| Pangani | 2,328 | 8,068 | 5,740 | **2.47** |
| Kipumbwi | 630 | 1,833 | 1,203 | **1.91** |
| Mkwaja | 870 | 270 | (600) | **(0.69)** |
| **Jumla** | **3,828** | **10,171** | 6,343 | **1.66** |
| **Iliyopakiwa** | | | | |
| Pangani | 7,158 | 11,004 | 3,846 | **53.73** |
| Kipumbwi | 14,400 | 12,475 | (1,925) | **(13.37)** |
| Mkwaja | 4,998 | 2,199 | (2,799) | **(56.00)** |
| **Jumla** | **26,556** | **25,678** | (878) | **(3.31)** |
| **Jumla Kuu** | **30,384** | **35,849** | 5,465 | **17.99** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa kipindi cha miezi sita Julai – Disemba 2024 ya mwaka wa fedha 2024/2025 Bandari ndogo za Pangani, Kipumbwi na Mkwaja zimeweza kuhudumia jumla ya Tani **35,849** sawa na asilimia **118** ya lengo la kuhudumia jumla ya **Tani 30,384**. Bandari ya Mkwaja ikihudumia jumla ya mifugo **17,955**.

### 18.3 Ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Hali ya ukusanyaji wa mapato katika Bandari hizi ndogo za Pangani, Mkwaja na Kipumbwi kwa kipindi cha miezi sita Julai-Disemba 2024 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

**Jedwali No. 2 Mapato**

| MIEZI | BANDARI | | |
|---|---|---|---|
| | PANGANI | KIPUMBWI | MKWAJA |
| Julai-Disemba 2024 | 141,472,801 | 97,211,473 | 43,238,862 |
| **Jumla** | **141,472,801** | **97,211,473** | **43,238,862** |
| **Jumla kuu** | | | **281,923,136** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa kipindi miezi sita Julai-Disemba 2024 mwaka wa fedha 2024/2025 Bandari za Pangani, Mkwaja na Kipumbwi zimeweza kukusanya jumla ya **TZS 281,923,136.00**

### 18.4 Mafanikio

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Mafanikio ambayo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeyapata ni kama ifuatavyo;

i. Kuongeza mapato ya Wilaya ya Pangani kupitia Bandari zilizorasimishwa ambazo ni Pangani, Kipumbwi na Mkwaja. Uwepo wa Bandari hizi umesaidia kuboresha maendeleo ya mteja mmoja mmoja na kupunguza uvujaji wa mapato ya Serikali.

ii. Kupeleka huduma za kibandari karibu na wananchi wa Pangani kwa kurasimisha Bandari ya Mkwaja na Kipumbwi zilizoanza kutoa huduma zake Mwezi Novemba 2019. Hapo awali wateja walikuwa wakienda Bandari ya Pangani au bandari ya Tanga.

iii. Imeongeza wigo wa ajira kwa wakazi wa Wilaya ya Pangani kwa kufanya kazi za kupakua na kupakia mizigo, usafirishaji wa mizigo kwa njia ya majahazi na makarani wa Bandari.

iv. Kuongezeka kwa ulinzi na usalama kutokana na doria zinazofanywa kudhibiti magendo na bidhaa zisizoruhusiwa kuingizwa nchini.

### 18.5 Changamoto na mikakati ya kukabiliana nazo

| NA | CHANGAMOTO | MIKAKATI |
|---|---|---|
| 1 | Mamlaka kukosa umiliki wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa miundombinu hasa kwa Bandari za Kipumbwi na Mkwaja | Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inaendelea kufanya tathimini ya utwaaji wa maeneo katika hizo Bandari. |
| 2 | Uwepo wa Bandari bubu ambazo bado hazijarasimishwa hupelekea kupunguza mapato ya Bandari zilizorasimishwa. | Kushirikiana na uongozi wa Serikali ya sehemu husika na pia kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutumia Bandari zilizorasimishwa. |

## 19.0 WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA (TFS)

### 19.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ofisi ya Mhifadhi misitu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Pangani. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi CCM, TFS – Pangani imetekeleza Kifungu namba 69 kwenye kifungu kidogo cha (c).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kifungu namba 69 kifungu Kidogo (c): **Kutekeleza mikakati ya kudhibiti ujangili wa wanyamapori, misitu na mazingira ya nyuki, kuimarisha ulinzi dhidi ya wanyamapori ili kulinda maisha ya wananchi na mali zao na kutatua migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Utekelezaji wa ilani hii umefanyika kwa kufaniksha kufanyika kwa doria za ulinzi wa misitu za nchi kavu Misitu ya Hifadhi wa Msubugwe wenye hekta 4,577.56, maeneo Mengine

ya wazi na za bahari Misitu ya Hifadhi ya Mikoko yenye hekta 1,750. Zoezi hili linafanyika kila Mwezi katika nyakati tofauti.

### 19.2 Utekelezaji wa ilani kwa Kipindi cha Julai hadi Disemba 2024.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Doria za Nchi kavu Jumla ya Doria **15 za kupangwa** na **60 za kila siku** za ulinzi wa nchi kavu zimefanyika katoka maeneo mbalimbali kama Vile Msubugwe, Mkalamo, Mseko, Masaika, Mkwaja, Mburizaga, Kipumbwi n.k. Doria za maji jumla ya doria **7 za Kupangwa** na **12 za Kila siku** na zilijikita zaidi katika bandari bubu zilizopo kando ya Bahari na Mto Pangani maeneo haya ni Kipumbwi Mtoni, Ushongo, Sange, Buyuni, Sima, Stahabu, Mkwaja, Matakani na Bweni.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Doria hizi zilifanikishwa kushikiliwa kwa vitu vifuatavyo: **Pikipiki 19**, gunia za **mkaa 320** zenye kilo 54 kila moja, **Trekta 1**, **Mifugo 336**, **Gari 1**, **Guta 1**, **Baiskeli 4**, Vipande vya **Mbao 76** aina ya Mpilipili (*warbugia spp)*, **Magogo 10** ya Mtiki, Vipande vya **Mbao** 34 aina ya Mfunda (*Zenkerella grotei)*, Vipande vya **Mbao 37** aina ya Msufi pori (*Bombax)*, Vipande vya **slipa 35** aina ya Mvule (*Millicia spp)*, Vipande vya **slipa 42** aina ya Msangazi (*Cassia abbreviate)* kwa Mchanganuo Ufuatao wa Kila Mwezi;

i. **Mwezi Julai**

**Idadi ya Doria**: Doria za Nchi kavu zilifanyika ni 3 za Kupangwa na 9 za Kila Siku na Doria za bahari 1 ya Kupangwa na 2 za kila siku.

Vitu Vilivyokamatwa: **Pikipiki 4**, gunia za **mkaa 171** zenye kilo 54 kila moja, Vipande vya **Mbao 22** aina ya Mpilipili (*warbugia spp).*

ii. **Mwezi Agosti**

**Idadi ya Doria**: Doria za Nchi kavu zilifanyika ni 3 za Kupangwa na 10 za Kila Siku na Doria za bahari 1 ya Kupangwa na 2 za kila siku.

Vitu Vilivyokamatwa: **Gari 1, Mifugo 157,** gunia za **mkaa 25** zenye kilo 54 kila moja, Vipande vya **slipa 35** aina ya Mvule (*Millicia spp)*, Vipande vya **slipa 42** aina ya Msangazi (*Cassia abbreviate)* na Vipande vya **Mbao 10** aina ya *warbugia spp.*

iii. **Mwezi Septemba**

**Idadi ya Doria**: Doria za Nchi kavu zilifanyika ni 3 za Kupangwa na 8 za Kila Siku na Doria za bahari 1 ya Kupangwa na 2 za kila siku.

Vitu Vilivyokamatwa: **Pikipiki 3,** gunia za **mkaa 23** zenye kilo 54 kila moja na **Mifugo 91.**

iv. **Mwezi Oktoba**

**Idadi ya Doria**: Doria za Nchi kavu zilifanyika ni 2 za Kupangwa na 9 za Kila Siku na Doria za bahari 1 ya Kupangwa na 2 za kila siku.

Vitu Vilivyokamatwa: **Pikipiki 4,** gunia za **mkaa 21** zenye kilo 54 kila moja, na Vipande vya **Mbao 14** aina ya Mpilipili (*warbugia spp).*

**v. Mwezi Novemba**

Idadi ya Doria: Doria za Nchi kavu zilifanyika ni 2 za Kupangwa na 11 za Kila Siku na Doria za bahari 2 ya Kupangwa na 2 za kila siku.

Vitu Vilivyokamatwa: **Pikipiki 4,** gunia za **mkaa 40** zenye kilo 54 kila moja, **Mifugo 88**, **Baiskel 3**, Vipande vya **Mbao 10** aina ya Mpilipili (*warbugia spp*) na **Magogo 10** ya Mtiki

**vi. Mwezi Disemba**

**Idadi ya Doria**: Doria za Nchi kavu zilifanyika ni 2 za Kupangwa na 13 za Kila Siku na Doria za bahari 1 ya Kupangwa 2 za Kila Siku.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Vitu Vilivyokamatwa: **Pikipiki 4, Trekta 1, Guta 1,** gunia za **mkaa 40** zenye kilo 54 kila moja, **Baiskel 3**, Vipande vya **Mbao 20** aina ya Mpilipili (*warbugia spp)*, Vipande vya **Mbao** 34 aina ya Mfunda (*Zenkerella grotei)*, na Vipande vya **Mbao 37** aina ya Msufi Pori (*Bombax).*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Vitu Hivi vilivyokamatwa kwa maana ya vyombo vya moto kma vile Gari, trekta na PIkipki vilihifadhiwa na wahusika walilipa tozo ya ufifilishaji baada ya kukiri makosa kulingana na sheria ya Misitu na kupatiwa vyombo vyaon na mazao ya Misitu yalifuata taratibu zingine za kisheria.

### 19.3 Mengineyo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Aidha Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya Tanzania (TFS) Wilaya ya Pangani inaazimia utekelezaji wa vifungu vingine vya Ilani kwa kipindi cha Mwezi Januari had Juni 2025 katika Kifungu cha 69 kifungu kidogo cha (g) katika suala zima la Kuendeleza programu mbalimbali za upandaji miti na ufugaji nyuki ili kutunza mazingira na kuongeza kipato kwa wananchi na Taifa. Kwani Tunaazimia kufanikisha upatikanaji wa miti 10,000 ya aina mbalimbali na tuko katika mpango mzima wa Kuwa na Bustani ya Miti itakayoweza kuzalisha miche 50,000 za miti ya aina mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Naomba kuwasilisha.

GIFT I. MSUYA
**MKUU WA WILAYA**

**PANGANI**